


# MUHURI WA SABA

 Asante, ndugu. Wakati tukiwa tumesimama, na tuombe.

<sup>2</sup> Mwenyezi Mungu, mwanzilishi wa Uzima, na mpaji wa thawabu zote njema, za kiroho, kweli tunashukuru sasa kwa ajili ya wakati huu wa ajabu sana, muhimu sana, wakati wa ushirika katika Uwepo Wako, unaonyesha sehemu muhimu sana maishani mwetu, Bwana, wakati ambao hatutasahau kamwe, haidhuru tutaishi muda gani. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba katika usiku huu wa mwisho. . . Tunaona Maandiko, katika siku ya mwisho ya sikukuu, Yesu alisimama kati yao na kupaza sauti, “Mtu akiona kiu, na aje Kwangu!” Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba jambo hilo litarudiwa tena usiku wa leo, ili kwamba tuweze kusikia Sauti ya Bwana wetu ikituita, na ikituita kuingia katika utumishi Wake, maisha ya kutembea karibu zaidi. Tunajisikia ya kwamba tumeisha sikia tayari Sauti Yake, katika kufunguliwa kwa Mihuri hii, ikinena ya kwamba ni siku ya mwisho, na wakati umekaribia. Tujalie baraka hizi tunazojiomba, Baba, katika Jina la Yesu Kristo, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

Ketini.

<sup>3</sup> Ningependa kuongezea jambo hili, ya kwamba, katika ibada zote nilizowahi kufanya maishani mwangu, ninaamini juma hili limekuwa ndio wakati wa fahari sana maishani mwangu mwote katika huduma. Haidhuru nina nini. . . Nimeona miujiza mikubwa ikitendeka, ndiyo, hapo nyuma, na ibada za uponyaji, lakini hili limezidi hayo. Umekuwa ni mmoja wa nyakati kuu sana, nyakati muhimu sana za maisha yangu, ni kuwa mahali hapa. Pia ninaona maskani hii ndogo ikichukua sura nyingine; si hilo tu, bali ndani kunatwaa sura tofauti!

<sup>4</sup> Na, sasa, nilikuwa nikimwuliza Billy; alichelewa sana, kuja kunichukua. Akasema kulikuwa na kundi lingine lililobatizwa likibatizwa. Ambapo, wanafikia kwenye mia moja, kwa juma hili, watu wanaobatizwa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa hiyo, tuna—tunashukuru. Na Mungu awabariki!

<sup>5</sup> Na, sasa, kama huna kanisa la nyumbani, tunakukaribisha uje hapa, kuja na kushiriki pamoja nasi. Kumbuka tu ya kwamba kanisa liko wazi. Sisi si madhehebu, nami ninatumaini na kuamini ya kwamba halitakuwa madhehebu hata. Ni ushirika tu ambapo wanaume na wanawake, na wavulana kwa wasichana, wanakutana kwenye meza ya Mungu, na kuwa na ushirika kwenye Neno, nasi tuna vitu vyote shirika.

<sup>6</sup> Sasa, nasi tuna mchungaji mzuri sana, mtu halisi wa Mungu, nami ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Kama utakumbuka, ono moja, mwaka mmoja uliopita, ya kwamba

Chakula kilikuwa kimewekwa akiba mahali hapa. Na hilo ni kweli kabisa. Nasi tunaninii . . .

7 Tuna mahali hapo sasa, pa kutosha, kwa ajili ya madarasa ya shule ya Jumapili, kwa ajili ya umri mbalimbali, nasi tunashukuru sana kwa ajili ya nafasi hii. Watu fulani wamesema, wakati mmoja, laiti wangelikuwa na madarasa ya shule ya Jumapili mahali ambapo wangewapeleka watoto wao. Sasa, ninyi, wao wanayo sasa. Kwa hiyo, sasa, kwa hiyo wewe njoo moja kwa moja tu na uwe pamoja nasi kama huna kanisa la nyumbani.

8 Bila shaka, kama unalo kanisa zuri ambalo unahudhuria, na linahubiri Injili, na kadhalika, mbona, hilo—hilo kwa kweli ni kundi lingine letu, unaona, mahali pengine. Lakini kama huna la nyumbani, nawe una- . . .

9 Nafahamu ya kwamba wengi walikuwa, wamehama kutoka sehemu nyingine nchini, kulifanya hili kuwa kanisa lao la nyumbani. Nasi kweli tunawakaribisha hapa kwenye Neno la Bwana. Nami ninakumbuka, nadhani, wakati nilipoondoka, niliwaambia ya kwamba—ya kwamba ibada, kadiri nihusikavyo mimi, zapaswa kuwa hapa maskanini.

10 Sijajua bado yale yote Bwana aliyoniwekea kwa siku zijazo. Ninamwachia jambo hilo mkononi Mwake, si ushirikina wa namna fulani wala cho chote kile. Ninamngojea tu, siku kwa siku, Yeye aniongoze mahali ambapo ningeweza kumtumikia Yeye vizuri zaidi. Na wakati Yeye atakapomaliza na mimi, basi ninaamini ya kwamba atanipokea Nyumbani, katika amani.

11 Na, sasa, ninashukuru sana kwa ajili ya ushirikiano wa watu wa maskani. Kama Billy alivyokuwa ananiambia juma hili, kwamba, nafikiri, kila nyumba iliyowakilishwa hapa karibu na maskani hii ina mtu wanayekaa nae. Wao waliweka wazi, nyumba zenu na sehemu mbalimbali, na kuwakaribisha watu ambao hawangekuwa na mahali pa kwenda. Sasa, hayo ni matendo halisi ya Kikristo. Na nyumba nyingine zimewaweka watu katika kila sehemu ndogo waliyoweza, kuwapatia watu mahali pa kukaa.

12 Kwa sababu, huu umekuwa ni wakati mgumu sana, kwa ajili ya jambo hili, jambo fulani ambalo limekuwa likiendelea, kuhusu ulimwengu wa riadha, namna fulani ya mpira wa kikapu ama cho chote kile, na—na vyumba vilikuwa vimekodishwa. Pamoja na kundi kubwa kutoka . . .

13 Nafikiri, wamewakilishwa hapa katika kanisa hili dogo, kama, kwenye majimbo ishirini na manane ama majimbo thelathini yamewakilishwa papa hapa kanisani, mbali na mataifa mawili ya kigeni, kwa hiyo, na ufufuo huu mdogo. Kwa hiyo, hilo linachukua nafasi kubwa sana, lenyewe. Mwajua juu ya . . .

14 Nilikuwa nikiuliza leo, pamoja na baadhi ya watu. Nilisema, “Nafahamu hakukuwa na watu wengi sana wa Jeffersonville hapa, kwenye mkutano.”

15 Mtu fulani akajibu, akasema, “Hatuwezi kuingia.” Vema, hilo, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Hiyo ilikuwa ndiyo sababu yake. Baadhi ya polisi, na kadhalika, walitaka kuja kwenye mkutano, lakini walisema, walikuwa wakizungumza hapa karibu, wakasema, lakini walikuja na hawakuweza kuingia, kwamba ilikuwa tayari imejaa hata kabla ya wakati wao kuweza kuingia. Kwa hiyo walikuwa na wakati wao, labda, baadaye, nao hawakuja. Kwa hiyo sasa watu wanakuja kutoka sehemu nyingine, kwa hiyo tunashukuru sana.

16 Sasa, sijui. Jambo linalofuata ambalo lingefuatia hili, lingekuwa ni zile Baragumu Saba, katika ujumbe mwingine. Lakini, katika ile Mihuri, kwa kweli kila kitu kimo humo ndani. Zile nyakati za kanisa zikaja, nasi tukaziweka za kwanza, ambazo zilikuwa ninii sana—ambazo zilikuwa ni za muhimu sana, lakini ninii...kwa wakati huo. Sasa, kufunguliwa kwa Mihuri kunaonyesha mahali ambapo Kanisa linaenda, na jinsi linavyoishia. Na sasa, nafikiri, Baba wa Mbinguni kweli amekuwa wa neema kwetu, kwa kuturuhusu kuona yale tuliyoona.

17 Nami ninasema jambo hili, nikiangalia ile mihitasari ya zamani niliyotumia kuhubiria, miaka mingi iliyopita, nilikuwa tu nikija na kusema yale niliyofikiria yalikuwa ni sawa, na kuendelea. Nilikuwa nimeenda mbali sana na jambo halisi. Na sasa, hiyo Mihuri yote minne, niliihubiri katika somo la kama dakika ishirini, yote. Wale wapanda farasi wanne, wa Ufunuo, niliwaweka wote pamoja na kusema, “Farasi mmoja alienda katika nyeupe,” nikasema, “labda huo ni ule—ule—ni ule wakati wa mwanzoni. Na farasi aliyefuata alitokeza kwenda katika njaa,” na halafu na kuendelea namna hiyo. Lakini, jamani, wakati Neno lilipofunguliwa hasa hasa, Hilo lilikuwa maili mia moja mbali kabisa nalo.

18 Kwa hiyo, inatubidi kuwa waangalifu na kungojea. Na labda ilipaswa iwe ni wakati huu wa kufanya jambo hilo. Huenda kumekuwa na mambo mengi ambayo yamesemwa, ambayo huenda yasikubaliwe na watu wengine. Lakini ninaamini, wakati ule mkuu wa kumalizia utakapokuja, nasi tukutane na Bwana wetu, utajakuta ya kwamba Hilo lilikuwa ni kweli. Ni—ni—ni kweli kabisa.

19 Sasa, watu ambao wametokea nje ya mji, kutoka sehemu mbalimbali, waliokuja kutoka katika majimbo mbalimbali na mataifa, jinsi ninavyofurahia uaminifu wenu kusafiri umbali wote huo, na kuchukua likizo zenu. Na wengine wao bila hata na mahali pa kukaa! Na—najua, maana nimeweza kuwasaidia wengine wao kupata mahali pa kukaa. Bila hata na pesa

za chakula, wala cho chote kile kingine, na kwa hiyo. . .na hata wanakuja, hata hivyo, wakitarajia jambo fulani kutukia, kushughulikia jambo hilo. Na wakiwa na imani kubwa namna hiyo kwamba, haidhuru kama itawabidi kukosa chakula, ama hata kukosa mahali pa kukaa, wanataka kuja kusikia hayo, mambo hayo yakitukia, hata hivyo. Huo ni ushujaa kweli, mwajua. Na kila mtu amekuwa hivyo asilimia mia moja!

<sup>20</sup> Nilikutana na shemeji yangu kule nyuma, aliyekuwa ni—ninii. . .aliyejenga matofali ya kanisa, na kadhalika. Nami nilikuwa nikimwambia jinsi nilivyofurahia kazi yake. Mimi si—mwashi wa matofali, wala sijui lo lote kuhusu hilo. Lakini ninajua kona mraba ni nini, na kama imewekwa sawasawa.

<sup>21</sup> Naye akasema, “Ngoja nikwambie.” Akasema, “Hapajawahi kuwapo na wakati kama huo, ni vigumu kuupata, ambapo mtu uliwahi kuona unoja wa namna hiyo kati ya watu, wakati watu wote wanapofanya kazi pamoja.”

<sup>22</sup> Ndugu Woods, Ndugu Roberson, na kila mtu wanaweka tu mahali pao, kila kitu. Na yule ndugu ambaye—ambaye aliweka vyombo vya kusikilizia, ninii. . .Ninamaanisha vyombo vya mawasiliano na kila kitu, kanisani. Wao walisema, “Kila kitu kilienda vizuri vile ilivyotakiwa.” Walipohitaji kitu fulani, kungekuwako na mtu huyo anayehitajika amesimama pale kufanya jambo hilo. Kwa hiyo ni ninii. . .Mungu yuko katika programu yote nzima. Tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili.

<sup>23</sup> Wadhamini wengi wakuu kanisani, kusaidia kufanya jambo hilo, kama vile Ndugu yetu Dauch na Dada Dauch wanaoketi hapa, na wengine wengi ambao wamechanga fedha nyingi kwa ajili ya jambo hili. Nami nafikiri, wakati uu huu, hawana hata kitu kidogo wanachokosa, na kila kitu kimelipiwa. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo.

<sup>24</sup> Kumbukeni, ni kanisa lenu, kwa kuwa wewe u mtumishi wa Kristo. Na hiyo ndiyo sababu limejengwa hapa, mlango ulio wazi wa kujenga watumishi, na kwa watumishi ambao tayari ni watumishi wa Kristo, kuingia na kufurahi kwenye ushirika wa Yesu Kristo. Na tunataka mjue ya kwamba kila mtu amekaribishwa.

<sup>25</sup> Na sasa mnaponisikia mimi wakati mwingine, wakati wa kuwa kwenye upako, kwa namna fulani nikirarua pazia la madhehebu, si—simaanishi hilo dhidi ya mchungaji wenu, wala dhidi ya ndugu ye yote, dada, kanisani. Kwa maana, hata hivyo, Mungu ana watu katika kila madhehebu yaliyopo. Lakini Yeye hayatambui madhehebu; Yeye anawakubali watu binafsi katika madhehebu. Na ninii. . .Haihitaji madhehebu fulani.

<sup>26</sup> Kwa hiyo, wakati watu wanapofungwa sana kwenye madhehebu, basi hawawezi kuona kitu kingine cho chote ila yale tu ambayo kanisa hilo linasema, unaona. Na hilo linakatiza ushirika na watu wengine, na ni utaratibu ambao Mungu

hapendezwi nao, na ni mambo ya kimwili ambayo Mungu hajapata kuyachagua kamwe.

<sup>27</sup> Kwa hiyo, sasa, simaanishi mtu ye yote binafsi. Mkatoliki, Myahudi, ye yote yule, ama—ama Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, madhehebu yo yote, bila madhehebu, na—na wasio wa kimadhehebu, na wengine wote, Mungu ana watoto Wake wanaoketi huko nje. Unaona? Na mara nyingi mimi ninaamini wako huko nje kwa kusudi fulani, kutoa Nuru, kuwavuta wale waliochaguliwa tangu zamani kutoka kila mahali. Na—na kwenye ile siku iliyo kuu, tutaona basi, Kanisa la Bwana Yesu Kristo litaitwa kwenye—kwenye ule wakati mkuu wa mkutano hewani, nasi tutapaa sote juu kwenda kumlaki. Nami—nami ninautazamia wakati huo.

Sasa, kuna mengi sana yangaliweza kusemwa!

<sup>28</sup> Na usiku wa leo, kwenye ule usiku wa mwisho, wa kumalizia, kama ilivyo kawaida, kila mtu ananinii. . . Katika ibada ya kuponya, ninaona, chini ya matarajio ya mambo makuu yatakayofanyika katika ibada ya oponyaji, ambayo huwafanya wahangaika, wawe na wasiwasi. Halafu ninaona jambo lile lile usiku wa leo, ya kwamba kila mtu yuko chini ya matarajio ya kuona jinsi. . . Na kila usiku, imekuwa namna hiyo, kwa ajili ya kufunguliwa kwa hiyo Mihuri.

<sup>29</sup> Sasa nataka kuliweka jambo hili wazi kabisa. Kila wakati, kila wakati ambapo Mihuri hii imefikia mahali; kila kitu nilichowahi kuamini juu Yake, na nimesoma kutoka kwa watu wengine, kimekuwa kinyume cha yale yaliyonijia mle chumbani.

<sup>30</sup> Na akili zangu, wakati huu. . . Sababu ya mimi kufanya ibada ile ya oponyaji asubuni hii, ni kwa sababu akili zangu za kibinadamu zinaenda mbali sana na mawazo yangu mimi mwenyewe. Nimejaribu kukaa kwenye—kwenye chumba fulani huku mapazia yamefungwa, na taa imewashwa. Hii ni siku ya nane. Na hata sijaingia kwenye gari langu, kwe—kwenda mahali po pote.

<sup>31</sup> Ilinibidi kwenda na baadhi ya ndugu fulani, benki, kutia sahihi hawala na kadhalika, zinazohusu fedha vitu ambavyo vilikuwa vimekopwa na kuazimwa na kanisa hili. Lakini ni—lakini nilirudi moja kwa moja, na kuanza moja kwa moja kusoma.

<sup>32</sup> Na jambo la ajabu, hapakuwapo na mtu hata mmoja aliyesema jambo lo lote. Ama, kwa kawaida, wao hubisha mlangoni, na kukutaka ufanye hili, na kila kitu. Hakujakuwapo na jambo hata moja. Imekuwa ni ajabu sana.

<sup>33</sup> Mahali nilipomekuwa nikilia chakula, ni kwa Ndugu Wood. Kwa kawaida mahali hapo huwa pamejaa magari. Nao walikuwa na watu wanane ama kumi ambao walikuwa waje wakakae nao kwa wakati huu, na hakuna hata mmoja wao aliyekuja.

<sup>34</sup> Halafu, asubuhi ya leo, sitasahau kamwe asubuhi ya leo, neema ya Mwokozi wetu kwa mtumishi Wake aliyechoka, mchovu. Wakati, nilikuwa nimejibu swali la maskini mtu mmoja, na, kwa akili zangu zote, nikidhania ya kwamba nilikuwa nimefanya vema. Na, mara, kana kwamba nilikuwa—nilikuwa nimemnyang’anya mtoto kitu fulani, nilikosa amani kabisa, wala sikujua ilikuwa ni kitu gani. Basi nikawaza, labda kwa sababu nilikuwa ninaharakisha kuanza ile ibada ya uponyaji, huenda mtu fulani ni mgonjwa taabani, ambaye ilibidi aombewe saa hiyo hiyo. Ndipo niliwauliza kusanyiko. Katika dakika chache, lilifunuliwa. Ndipo mtu fulani akasema, “Mbona usisome ninii yako—usisome kifungu chako tena?” ama kitu kama hicho. Na wakati huo huo, nikaokota kile kijikaratasi na kukisoma tena, kuona kilisema nini. Basi nikaangalia kwenye Kitabu, na lilikuwa ni jambo tofauti kabisa, lile swali nililokuwa ninajibu. Unaona?

<sup>35</sup> Hebu niwajulisheni tu jambo hili. Wakati ya Kimbinguni yanapoingia, hiyo ni nia ya Kristo. Unakuwa mbali sana na mawazo yako mwenyewe, mpaka, katika nia yako mwenyewe, mimi. . . Hili, wewe. . . Sininii. . . Msiache nijaribu kuelezea mambo hayo, kwa sababu siwezi. Unaona? Nisingeweza kuelezea jambo hilo. Hakuna mtu angeweza kulielezea.

<sup>36</sup> Mtu huyo angewezeje, huyo ni Eliya, asimame kule juu ya mlimani, chini ya Uwepo wa Mungu, na ashushe moto kutoka mbinguni, halafu mvua moja kwa moja nyuma ya ule moto? Halafu afunge mbingu, wala haikunyesha kwa miaka mitatu na miezi sita, halafu anarudi moja kwa moja na kuita mvua, katika siku iyo hiyo! Na chini ya upako huo, vipi. . . Halafu akawachukua makuhani mia nne akawapeleka huko na kuwaua; na halafu akakimbilia nyikani, akipiga mayowe kwa ajili ya uhai yake, kwa tishio la mwanamke mmoja. Unaona? Yezebeli, yeye aliapa ya kwamba angemwua. Wakati, Ahabu na hao wote walipokuwa pale, kuona Uwepo wa Mungu na mwujiza mkuu uliofanywa. Unaona, ninii yake. . . Roho alikuwa amemwacha. Katika namna yake ya kuwazia ya kawaida, yeye hakujiwa na mawazo yo yote, unaona. Hakuweza kuwaza.

<sup>37</sup> Na, kumbukeni, yule Malaika alimlaza usingizi, na akampumzisha. Akamwamsha, akampa mikate; kisha akamrudisha usingizini, na akampumzisha; halafu akamwamsha, akampa mikate tena. Nasi hatujui kilichompata mtu huyo, kwa siku arobaini. Halafu akaingizwa kwenye pango fulani, mahali fulani, ndipo Mungu akamwita.

<sup>38</sup> Usijaribu kueleza hayo ya Kimbinguni. Huwezi kuyaelezea. Unaona? Jambo tu unalopaswa kufanya, ni kwenda mbele tu moja kwa moja. Nami hujaribu kujiweka wazi niwezavyo, lakini tangu sasa nitaninii. . . nafikiri sitajaribu jambo hilo tena. Mtaamini tu kabisa, ama la. Nami ninaninii. . . Mtaona, baadaye kidogo, ni kwa nini.

Sasa, nimejaribu kuwa mwaminifu. Mungu anajua jambo hilo.

<sup>39</sup> Na lile swali asubuhi ya leo. Nilikuwa nikijaribu kulijibu kwa uaminifu kabisa tu nilivyojua namna ya kulijibu. Nilisoma tu sehemu ya kwanza ya kile kifungu, na ilikuwa ninii... isingekuwa ni sahihi. Lakini Roho Mtakatifu, akifahamu ya kwamba mimi... nia yangu... Unaona, angalia, siku mbili ama tatu zilizopita, yale yaliyokuwa yakitukia. Unaona, ni—niliita mia saba,... “elfu saba,” mia saba. Asubuhi ya leo, nilikuwa nikijaribu, na watu wakalitambua, unaona, na hilo lilionyesha ya kwamba ninii mlikuwa macho. Sasa, jambo lingine, mahali nilipokuwa nikijaribu kusema “hua,” nami nikaita ni mwana-kondoo; lakini nililikamata hilo pale pale. Na halafu, hapa, moja ambalo sikulishika katika jambo hilo, Roho Mtakatifu aligeuka moja kwa moja na kunielekeza kwenye hilo.

<sup>40</sup> Hilo ni dhahirisho maradufu ya kwamba mambo haya ni ya kweli. Ni ninii... Mungu anaangalia, kuona kwamba jambo Hilo ni sahihi. Hiyo ni kweli. Yeye anataka kufanya hivyo. Anawataka ninii mjue ya kwamba ni Kweli.

<sup>41</sup> Yeye ndiye anayelileta Hilo, maana hakika haikuwa... Imekuwa ni funzo kwangu, la kutosha, kama vile ilivyokuwa kwenu. Na kwa hiyo tunaninii mno... Ninashukuru kwa ajili ya maarifa ha—ha—hayo, kujua sasa kutoka kwa Bwana, ni wakati gani tunaoishi; unaona, tukiwa twaishi kabisa kabisa katika wakati wa mwisho, kabla ya kuondoka kwa Kanisa. Sasa ninii tu... .

<sup>42</sup> Tumekuwa tukizungumza, kwa hiyo hebu na tuombe baraka Zake juu ya Neno tena.

<sup>43</sup> Baba yetu wa Mbinguni, huu hapa waja usiku ule mkubwa, saa kuu hiyo ambapo jambo kubwa limetukia. Limekuwa karibu na watu wakati wote. Na, Baba, naomba ya kwamba usiku wa leo litajulikana, bila shaka hata kidogo, kwenye mioyo ya watu na nia zao, kwamba waweze kujua ya kwamba Mungu angali yuko kwenye Kiti cha Enzi, na ya kwamba Yeye angali anawapenda watu Wake.

<sup>44</sup> Na ndiyo ile saa, saa ambayo ulimwengu umetamani kuiona, sasa inakaribia, kwa sababu inalilia ukombozi. Tunaweza kuona vitu vya asili vikiwa tayari kuirudisha. Tunaweza kuona vitu vya asili vikiwa tayari kulileta Kanisa katika Uwepo wa Kristo. Tunaweza kuona Bi—Bibi—arusi akiumbika, akivaa nguo ya arusi, akijifanya tayari. Tunaweza kuona vimulimuli. Tunajua ya kwamba tuko mwisho.

<sup>45</sup> Sasa, Baba wa Mbinguni, wakati hili linapojitokeza mbele sasa kuhubiri, ama kufundisha juu ya tukio hili kuu, na lenye nguvu nyingi lililotukia Utukufuni, miaka elfu mbili iliyopita, na likapewa, yule mtume mkuu anayependwa, Yohana. Na usiku wa leo tunazungumza juu ya jambo Hilo. Jalia Roho Mtakatifu aje

sasa katika uwezo wa Nguvu Zake kuu za ufunuo, ili kwamba apate kutufunulia jambo lile ambalo anatutaka tujue, kama alivyofanya katika siku chache zilizopita usiku. Tunajikabidhi Kwako, pamoja na Neno, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>46</sup> Sasa, kama mnataka kufungua, labda, katika Biblia zenu. Na hii ni aya fupi tu, aya moja ya Maandiko. Lakini ndiyo aya ya mwisho, inayopatikana . . . Muhuri wa mwisho, hasa.

Sasa, usiku wa jana tulikuwa tukizungumza juu ya Muhuri wa Sita.

<sup>47</sup> Muhuri ya Kwanza, ukiwa ni kutambulishwa kwa mpinga-Kristo. Wakati wake ulikwisha, nasi tuliona jinsi alivyotoka.

<sup>48</sup> Jinsi yule Mwenye Uhai alivyotambulishwa, katika Nguvu za Mungu zilzotoka kwenda pamoja na nguvu za mpinga-Kristo, kukabiliana naye! Siamini kungeweza kuwa na swali katika nia ya mtu ye yote juu ya jambo hilo.

<sup>49</sup> Ndipo tunaona, ni mara baada ya jambo hilo, ambapo, wakati ule wa kanisa, hao Wenye Uhai walitoka.

<sup>50</sup> Tukapitia, tunaona, tulibadilisha, picha yote nzima pale, hakuna Wenye Uhai wengine tena waliotoka. Unaona? Lakini, ilikuwa ikitambulisha, ikisonga mbele, kuingia kwenye wakati wa ile Dhiki, baada ya Kanisa kuondoka.

<sup>51</sup> Jinsi ilivyolingana kabisa na zile nyakati za kanisa! Sioni nukta moja, jambo moja ambalo halikukubaliana kikamilifu, hata kwa zile nyakati na kila kitu, na majira. Wazia jambo hilo. Hiyo inaonyesha, ilibidi iwe ni Mungu aliyetenda jambo hilo. Akili za mwanadamu hazingeweza kutambua jambo hilo. Na sasa tunatambua ya kwamba jambo hilo, pia, sisi . . .

<sup>52</sup> Bwana alitujalia kuchukua Maandiko, Maandiko Matakatifu, yale Yesu aliyosema yangetukia. Nasi tungaliwezaje kupata jambo hilo? Na hapa, anakuja na kufunua, na kulileta vile vile kabisa. Mahubiri Yake pale, yakijibu jambo hilo, yanaeleza jambo hilo barabara kabisa, sita kati ya hiyo Mihuri, lakini Yeye aliuacha wa Saba. Unaona?

<sup>53</sup> Halafu wakati Mihuri ilipofunguliwa, Mungu, angalia hapa, Yeye hata hakufunua mfano wo wote wa Ule wa Saba. Mnaona? Ni siri kabisa ya Mungu. Angalia. Sasa tutasoma katika Biblia, katika—katika Muhuri wa Saba. Huo unapatikana katika Ufunuo sura ya 8.

*Hata alipoifungua muhuri ya saba, kukawa kimya mbinguni kama muda wa nusu saa.*

<sup>54</sup> Na hayo tu ndiyo tuliyo nayo juu ya huo. Sasa tutaona.

<sup>55</sup> Na nitajaribu nisikawie sana, maana wengi wenu watakuwa wakisafiri, tayari, usiku wa leo, wakienda nyumbani. Nami nilifikiria tena, nifanye ibada ya uonyaji asubuhi ya leo, jambo



ambalo lingewaacha mwondoke asubuhi, haitawabidi kungojea. Na sasa sisi . . .

<sup>56</sup> Nami, pia, sina budi kusafiri mpaka—mpaka Tucson, Arizona, ambako ninaishi. Na ndiyo nyumbani kwangu sasa. Na halafu na—nataka kurudi hapa, Bwana akipenda, kwenye . . . Jamaa yangu inataka kurudi kwa siku chache Juni. Na, basi, huenda nitakutana nanyi nyote hapa, kutakuwa na mkutano wakati huo.

<sup>57</sup> Ibada yangu nyingine iliyopangwa ni Albuquerque, New Meksiko. Ninafikiri ni tarehe tisa, kumi, na kumi na moja. Nitakuwako kule Alhamisi na Ijumaa Kuu. Kwa hiyo, nilitaka nizichukue zote nzima, nami nilikuwa na maagano mengine ambapo nisingeweza kuyatimiza mpaka wakati huo, kwa hiyo nitakuwa na Alhamisi usiku na Ijumaa usiku, huko Albuquerque, New Meksiko.

<sup>58</sup> Na kisha—na kisha u—unaofuatia pili, unaojulikana, karibu, ni kwa uwezekano. Hatuna hakika kabisa. Huo nitakuwa pamoja na marafiki wangu wema, lile—lile kundi la *Kilio cha Usiku wa Manane*, huko . . . huko Southern Pines, Carolina ya Kaskazini.

<sup>59</sup> Nao wako kwenye simu kule sasa, ambapo, wametuma telegramu, ujumbe, na kila kitu, na nikiwa nimekuja karibu sana hivi, kwa manufaa ya kundi lingine, huko Little Rock; la watu wa Jina la Yesu ambao nilikuwa na mkutano nao, huko Cow Palace kwenye majira yaliyopita ya kiangazi. Wao wanafanya mkutano wao huko Little Rock, Arkansas. Nao wamekuwa, tangu mwaka uliopita, wakitamani angaa usiku mmoja. Ama, wanatamani wote, lakini hata wangukuwa tayari kupata usiku mmoja. Na kwa hiyo niliwaambia, nikiwa sijui la kufanya, nilisema wao wanaweza kuutangaza, “kwa matarajio.” Halafu watautangaza baadaye kidogo.

<sup>60</sup> Je! yeye amepiga simu sasa hivi? A—ha. Vema. Ati nini? [Ndugu fulani anasema, “Hot Springs.”—Mh.] Hot Springs, sivyo? Nilikosea. [“Ishirini na nne.”] Tarehe ishirini na nne mwezi wa . . . [“Mei”] Mei? [Mtu fulani anasema, “Ishirini na nne mpaka ishirini na nane Juni.”] Ishirini na nne mpaka ishirini na nane Juni. Sasa imetangazwa, “Kwa uwezekano,” yaani, “kama ni mapenzi ya Bwana.” Mnaona? Nitaninii . . .

<sup>61</sup> Hii hapa ndiyo sababu ya mimi kutaka kufanya mambo hayo. Mtajua baadaye kidogo, sasa, unaona. Ninapoenda mahali fulani, ninapenda kukanyaga kwa miguu yangu chini pale, nikijua ya kwamba Mungu alisema, “Nenda kule.” Basi kama adui akiinuka mahali po pote, ninasema, “Niko hapa katika Jina la Bwana Yesu. Hebu rudi nyuma!” Unaona? Unaona? Unaona? Nawe una—una hakika, mahali pako, unaona. Alipokutuma mahali po pote, Yeye atakuangalia. Unaona? Lakini kama ukienda, kwa kudhania, basi sijui; huenda Yeye asiwepo huko. Kwa hiyo na—nataka kuwa na hakika niwezavyo kuwa.

Nimeendesha mingi ambayo Yeye hakuniambia nifanye, lakini na—napenda kuwa na hakika iwezekanavyo. Bwana awabariki ninyi nyote sasa.

<sup>62</sup> Sasa, sasa tunaona, hiki kikiwa ni kifungu kimoja tu hapa, tungetaka kufanya kitu fulani kidogo—kidogo tu kabla ya hapa. Mnaona, tuliruka mlango wa 7. Mlango wa 6 unamalizia wa Sita, Muhuri wa Sita. Lakini, kati ya Muhuri wa Sita na Muhuri wa Saba, kuna jambo fulani linalotukia. Unaona? Na jinsi—jinsi hilo lilivyowekwa vizuri mahali pake sawasawa, kati ya, mlango wa 6 na wa 7. Sasa unaona katika mlango wa 7, tunaona, kati ya wa Sita na wa Saba, kuna pengo. Pengo, katikati, mlango wa 6 na wa 7 wa Kitabu cha Ufunuo, na ni kati ya Muhuri wa Sita na wa Saba ambapo pengo hili limetolewa. Sasa tunataka kuangalia jambo hili. Ni jambo muhimu sana kwamba tuangalie kipindi hiki kifupi.

<sup>63</sup> Sasa kumbukeni, baada ya mlango wa 4 wa Ufunuo, Kanisa limeondoka. Baada ya wale—wale wapanda farasi wanne kutoka, Kanisa limeondoka. Unaona? Kila kitu kilichotukia kwa Kanisa, kilitukia mpaka kwenye mlango wa 4 wa Kitabu cha Ufunuo. Kila kitu kilichotukia katika safari ya mpinga-Kristo, kiliendelea mpaka mlango wa 4. Na ule Muhuri wa Nne wa Ufunuo, kwa mpinga-Kristo na Kristo pia, ulimalizika. Na mpinga-Kristo anafikia maangamizi yake, na pamoja na jeshi lake; Na Kristo anakuja pamoja na jeshi Lake.

<sup>64</sup> Ni vita vya kale vilivyoanza huko nyuma kabisa, kabla ya wakati. Na halafu walikuwa. . . Shetani na malaika zake walifukuzwa, na ndipo wakaja duniani. Ndipo vita vikaanza tena, kwa sababu Hawa alivunja ile ngome kutoka mahali ambapo alitengwa, nyuma ya Neno la Mungu. Na tangu saa iyo hiyo, Shetani alishinda vita dhidi ya Neno la Mungu, kwa sababu mmoja wa raia Zake, yule aliye mnyonge zaidi, aliachia milango wazi. Na hivyo ndivyo hasa alivyoshinda vita kila wakati, imekuwa ni kwa sababu mmoja wa raia Zake aliacha mlango wazi kutoka kwenye Neno.

<sup>65</sup> Na jambo hilo lilitendeka katika wakati huu wa mwisho wa kanisa, kupitia kwenye utaratibu wa kimadhehebu. Ambao, kanisa halisi, la kweli, takatifu, la Mungu aliye hai, likiwa na mpanda farasi mwongo, halingekubali Neno, na akaligeuza kanisa kutoka kwenye Neno na kuliingiza kwenye fundisho la sharti.

<sup>66</sup> Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba kanisa Romani Katoliki limejengwa juu ya fundisho la sharti? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! wao wanakubali jambo hilo? Kabisa. Hakika. Bila shaka, wao wanalikubali. Isitoshe. Wakatoliki, hakika, halitawaudhi hata kidogo, kwa sababu wao wanajua jambo hilo. Wameongeza lingine jipya hivi karibuni, hapa si muda mrefu uliopita, ya kwamba Mariamu alifufuliwa.

Mnakumbuka hilo, hapa miaka michache iliyopita, yapata miaka kumi. Ni wangapi wanakumbuka hilo? ["Amina."] Gazetini, humo. Hakika. Mnaona? Kila kitu, lile "fundisho jipya la sharti." Unaona, lote ni fundisho la sharti, si Neno. Unaona?

67 Kasisi mmoja, kwenye mahojiano hivi majuzi, alisema, "Bw. Branham," akasema, "Mungu yuko katika kanisa Lake."

Nikasema, "Mungu yuko katika Neno Lake."

Akasema, "Hatupaswi kubishana."

68 Nikasema, "Mimi sibishani. Ninatoa tamshi tu. Mungu yuko katika Neno Lake. Hiyo ni kweli. 'Mtu ye yote ambaye ataondoa lo lote Kwake, ama kuongeza lo lote Kwake,' Neno lilisema."

69 Akasema, "Vema, Mungu alilipa... Kristo alilipa Kanisa Lake nguvu, na kuwaambia: lo lote walilolifunga duniani, litafungwa Mbinguni; na lo lote..."

Nikasema, "Hiyo ni Kweli kabisa."

70 Akasema, "Sisi tunayo, kwenye... kwenye kanuni hii, kwamba tuna nguvu za kufungua dhambi."

71 Ndipo nikasema, "Kama mkifanya jinsi lilivyotolewa kwa Kanisa, na jinsi walivyotekeleza jambo hilo, nitalikubali. Kama unalikubali, kuna maji hapa, 'kubatzwa katika Jina la Yesu Kristo upate ondoleo la dhambi zako,' unaona, si kwa mtu fulani kukwambia dhambi zako zimeondolewa." Unaona? Unaona? Hiyo ni kweli kabisa.

72 Mwangalie Petro akiwa na zile funguo, Siku ya Pentekoste. Kumbuka, yeye ana zile funguo ambazo wananena habari zake. Nao—nao hao watu wakasema, "Wanaume na ndugu zangu, tufanye nini tupate kuokolewa?"

73 Petro akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo" (kwa ajili gani?) "mpate ondoleo la dhambi, ndipo mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hilo linatatua jambo hilo milele. Limekwisha. Hilo lilitosha.

74 Sasa, lakini, unaona, mpinga-Kristo akaingia, kama tulivyolionyesha na kulielezea. Ni ufunuo wa ajabu jinsi gani! Jamani, jamani! Na kuwazia, miaka yote hii, tuliona likisonga mbele. Na ndio hili hapa kabisa, moja kwa moja, BWANA ASEMA HIVI.

75 Sasa, na tunaona kipindi hiki sasa, katikati, ya mlango wa 6 na wa 7. Sasa, mlango wa 7 wa Ufunuo, huu hapa u—u... unafunua tukio fulani. Haupo hapa bure. Haukuwekwa hapa, katikati ya hii, bure. Unaona? Uko hapa kwa makusudi fulani, na ni ufunuo unaofunua jambo fulani. Angalia jinsi unavyolingana

kiajabu na jinsi kimahesabu unavyokubaliana vizuri katika Maandiko! Unaona? Vizuri kabisa.

<sup>76</sup> Je! mnaamini katika hesabu za Mungu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama huamini, hakika umepotea katika . . . Hakika utapotea kwenye Neno, kama ukianza kuweka nne ama sita, ama—ama jambo fulani, mbali na maneno ya kihesabu yakiambatana kwa utaratibu. Hakika katika picha yako, utakuwa na ng’ombe anayekula nyasi juu ya mti, mahali fulani. Hakika utaishiwa. Kwa sababu, Mungu haninii . . . Neno Lake lote linakwenda kabisa katika—katika—katika mahesabu. Naam, bwana. Ni kamilifu, ni kamilifu kuliko vyote! Hakuna vitabu vingine vilivyoandikwa kama Hicho, kama Hicho, kamilifu sana katika he—hesabu.

<sup>77</sup> Sasa, m—mlango wa 8 unaonyesha tu picha ya—picha ya Muhuri wa Saba, ambapo hakuna kitu kingine kilichofunuliwa, sasa, hakuna kitu. Hakijafunuliwa katika Muhuri wa saba . . . sasa, hauna uhusiano wo wote na mlango wa 7 wa—wa Ufunuo. Kufunuliwa kwake, kwa Muhuri wa Saba, ni kimya kabisa. Na laiti ningalikuwa na wakati . . . Nitajaribu mahali pachache, kuwaonyesha.

<sup>78</sup> Huko nyuma kote, kutoka Mwanzo, mla . . . huu wa Saba ama Muhuri huu wa saba u—u—umezungumziwa. Tangu mwanzo kabisa, katika Mwanzo, Muhu . . . huu wa Sab- . . .

<sup>79</sup> Mihuri hii ilisafiri moja kwa moja kwenda mbele. Je! hamkuweza kukumbuka, asubuhi ya leo, nilipozungumzia mambo haya? Basi angalieni, usiku wa leo, nikiyazungumza. Nanyi mtaona, inapofikia kwenye huo Muhuri wa Saba, unakatika. [Ndugu Branham alidata kidole chake mara moja—Mh.] Naam.

<sup>80</sup> Yesu Kristo, katika kunena, Yeye Mwenyewe, alinena habari za wakati wa mwisho. Na wakati alipofikia . . . Alinena habari za Mihuri yote sita. Wakati alipofikia kwenye wa Saba, alinyamaza. Haya basi, unaona. Ni jambo kuu sana.

<sup>81</sup> Sasa, sasa, tunaenda kuzungumza hapa sasa juu ya sura hii ya 7, dakika moja tu, kwa—kwa namna fulani kuiunganisha, kati ya Muhuri wa Sita na wa Saba. Kwa sababu, hicho ndicho kitu tu tulicho nacho cha kufuatilia, sasa hivi, ni wa Sita . . . kati ya Muhuri wa Sita na wa Saba, ni kule kuitwa kwa Israeli.

<sup>82</sup> Sasa, nina marafiki wengi wazuri Mashahidi wa Yehova walioketi hapa, ambao wote . . . ama walikuwa Mashahidi wa Yehova. Labda wengine wao wangali ni Mashahidi wa Yehova. Lakini daima wameshikilia, Bw. Russel aliyashikilia, hawa mia na arobaini na nne elfu, kwamba ni Bibi—arusi wa kimbinguni wa Kristo. Unaona? Wao . . . Sivyoy ilivyo.

<sup>83</sup> Hawana uhusiano wo wote na wakati wa kanisa, hata kidogo. Wao ni Israeli kabisa. Sasa, tutasoma katika muda wa dakika chache. Sasa, pengo hili, kati ya ule wa Sita . . . ule

Mihuri, ni kuitwa na kutiwa muhuri kwa wale Wayahudi mia na arobaini na nne elfu, walioitwa katika ule wakati wa ile Dhiki, baada ya Kanisa kuondoka. Mnaona? Haina uhusiano wo wote na wakati wa kanisa, hata kidogo. Loo! wanaitwa, na inapatana vizuri kabisa na Maandiko. Yale majuma matatu na nusu ya mwisho ya Danieli, yaliyowekewa “watu” wa Danieli, unaona, si Mataifa. Kwa “watu” wa Danieli, na Danieli alikuwa Myahudi!

<sup>84</sup> Sasa angalia, Israeli, Israeli anaamini manabii wake tu, na ni, baada ya wao kuthibitishwa.

<sup>85</sup> Na hakuna mahali po pote katika wakati wa kanisa, tangu katika wakati wa mwanzoni mwa Kanisa la mitume, ambapo kanisa la Kiprotestanti liliwahi kuwa na nabii. Niambi eni alikuwa ni nani, na mnionyeshe. Kamwe! Walikuwa naye, katika wakati wa mwanzoni wa mitume, mmoja aliyetwa Agabo, ambaye alikuwa ni nabii aliyethibitishwa. Lakini katika... Wakati Mataifa walipoingia, katika urithi wa Mungu, na Paulo akawageukia Mataifa. Baada ya Petro, kama tulivyosoma jana usiku, kuwa amepokea kutoka kwa Bwana, ya kwamba, “Alikuwa anawachukua wa—watu kutoka kwa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake, Bibi—arusi Wake,” basi wao hapajakuwapo, katika kurasa za historia, nabii Mmataifa. Sasa rudi tu katika historia uone. Mbona? Kweli kabisa, ingekuwa ni kinyume cha Neno. Kweli kabisa.

<sup>86</sup> Wakati wa kwanza alipotoka, alikuwa ni simba, hilo lilikuwa ni Neno la nabii.

Wa pili aliyetoka, alikuwa ni kazi, dhabihu.

Aliyefuata, alikuwa ni werevu wa—wa mwanadamu.

<sup>87</sup> Lakini tumeahidiwa, katika siku ya mwisho, jambo hilo kurudi kwenye Kanisa tena, kwa manufaa ya kunyosha yote ambayo yamepotezwa, yamekosekana, hayakutekelezwa, yaliyoachwa bila kutekelezwa. Kwa maana, imetabiriwa hapa ya kwamba Ujumbe wa Malaika wa Saba ungemaliza zile siri za Mungu. Na, halafu tumepitia katika Hayo yote. Tunaona ya kwamba yanapatana kabisa na Maandiko. Hiyo ndiyo sababu yake.

<sup>88</sup> Sasa, ungeweza kuwazia, wakati mtu huyu atakapokuja jukwaani? Wakati atakapokuja, kumbukeni, litakuwa jambo nyenyekevu sana na kadhalika, hata makanisa yatalikosa kwa mbali sana. Na je! ungeweza kuwazia, makanisa, yakiwa yangali yako chini ya mapokeo ya watengenezaji, yangekubali kumpokea nabii kutoka kwa Mungu, ambaye angekuwa anayapinga vikali mafundisho yao pamoja na madhehebu yao?

<sup>89</sup> Sasa, kuna mtu mmoja tu ambaye angeweza kutimiza jambo hilo, Roho moja tu iliyopata kuwa duniani, niijuayo. Aidha ingekuwa... Itabidi iwe ni ya Eliya, katika wakati wake. Na ilibashiriwa kwamba ingekuwako, ambayo si kitu ila ni Roho wa Kristo.

90 Wakati Kristo alipokuja, Yeye alikuwa ni utimilifu. Alikuwa ndiye Nabii yule. Alikuwa Mu—Mungu wa manabii. Unaona? Unaona?

91 Kristo, angalia jinsi walivyomchukia. Lakini Yeye alikuja jinsi vile hasa Neno lilivyosema angekuja. Lakini kwa kuwa Yeye alikuwa ni Nabii, wao walikufuru hata wakajitoa katika Ufalme wa Mungu, kwa kumwita Roho wa Mungu, ambaye alikuwa akipambanua na kadhalika, “pepo mchafu.” Kasema, “Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni mpiga ramli, ama ibilisi,” ni huyo.

92 Mpiga ramli ni ibilisi, unaona, roho ya Ibilisi. Ndiyo. Mlijua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kabisa. Kupiga ramli ni kumwiga nabii, jambo ambalo ni kukufuru kabisa mbele za Mungu.

93 Sasa angalia. Wanaitwa, inakubaliaana vizuri kabisa na Maandiko, ya ile miaka mitatu na nusu ya mwisho ya Danieli.

94 Angalia, mwaamini—waamini wa Israeli wanaambiwa tu, katika Agano la Kale, kuamini manabii wao baada ya huyo nabii kuthibitishwa. “Kama kuna mtu kati yenu, ambaye ni wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana Mwe- . . . Mungu wako nitajijulisha Mwenyewe kwake, na kunena naye katika maono, katika ndoto, kufasiri ndoto.” Mtu fulani akiwa na ndoto, nabii ataweza kuifasiri. Na kama—kama ana ono, analinena. “Nitajijulisha Mwenyewe kwake kwa maono na ndoto, nitajijulisha Mwenyewe. Na kama yale asemayo yakitimia, basi msikieni nabii huyo, maana Mimi niko pamoja naye. Kama hayatimii, basi msimwogope kamwe. Naam. Hiyo ni kweli. “Ondokeni, achaneni naye, unaona.” Sasa hiyo ni . . .

95 Sasa, Israeli daima wataamini jambo hilo. Nanyi hamwoni? Kwa sababu gani?

Sasa nawatakeni mshike somo hili vizuri, usiku wa leo, sasa.

96 Kwa nini? Kwa sababu, hiyo ni amri kutoka kwa Mungu, kwao. Sijali ni vitini vingapi ambavyo Mataifa wanaweza kupeleka huko na kusambaza. Sijali utapitia Israeli mara ngapi ukiwa na Biblia kwapani mwako, ukithibitisha *hili, lile*, ama *lingine*, wao hawatapokea kitu ila nabii. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa maana, nabii ndiye tu ambaye angaliweza kulichukua Neno la Mungu na kuliweka Hilo katika mahali Pake, na kuwa nabii aliyethibitishwa. Wao wataamini jambo hilo. Hiyo ni kweli.

97 Kama nilivyokuwa nikizungumza na Myahudi hapa Benton Harbor, wakati yule John Rhyn, akiwa kipofu maishani mwake mwote, karibu, macho yake yalifunguka. Walinipeleka kule, huko kwenye nyumba ya Daudi. Na huyu rabi akatokea na ndevu zake ndefu. Akasema, “Ulimfungua John Rhyn macho yake kwa mamlaka gani?”

Nikasema, “Katika Jina la Yesu Kriso, Mwana wa Mungu.”

98 Akasema, “Pishilia mbali Mungu kuwa na Mwana!” Unaona? Kisha akasema, “Ninyi watu hamwezi kumkata Mungu katika vipande vitatu na kumpa Myahudi. Kufanya Miungu watatu kutoka Kwake; ninyi ni kundi la makafiri!”

99 Nikasema, “Mimi simkati Yeye katika vipande vitatu.” Nikasema, “Rabbi, je! lingekuwa ni jambo geni kwako kuamini mmoja wa manabii wenu alisema jambo fulani la uongo?”

Akasema, “Manabii wetu hawasemi uongo.”

Nikasema, “Isaya 9:6 ilikuwa ikinena juu ya nani?”

Akasema, “Masihi.”

100 Nikasema, “Basi, Masihi atakuwa Nabii-Mtu. Hiyo ni kweli?”

Akasema, “Ndiyo, bwana. Hiyo ni kweli.”

101 Nikasema, “Nionyeshe mahali ambapo Yesu alikosa kulitimiza.” Akasema. . . Nikasema, “Huyo Masihi-Nabii atakuwa na uhusiano gani kwa Mungu?”

Akasema, “Atakuwa Mungu.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli. Sasa umelipatia kwenye Neno.”

102 Nasema kweli, huyo Myahudi akiwa amesimama pale na machozi yakitiririka mashavuni mwake, akasema, “Nitakusikiliza baadaye kidogo.”

Nikasema, “Rabi, unaamini jambo hilo?”

103 Na akasema, “Angalia,” akasema, “Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu wana.” Nilijua alikuwa akizungumzia Agano Jipya.

Nikasema, “Kweli, Rabi! Sasa vipi kuhusu jambo hilo?”

104 Akasema, “Kama ningalihubiri jambo hilo, ningekuwa chini huko,” mnajua mahali pao ambapo pamekaa kwenye kilima pale, “chini kule mitaani, nikiomba riziki yangu.”

105 Nikasema, “Afadhali niwe chini kule nikiomba riziki yangu.” Mikono ya Myahudi bado ingali iko kwenye pesa, unajua. Unaona? Unaona? “Afadhali. . .” Na jina lake limeandikwa kwenye dhahabu, kwenye ile. . . Nikasema, “Afadhali niwe kule chini, nikila mikate migumu yenye chumvi nyingi na kunywa maji ya matawi ya miti, na nijue ya kwamba nimepatana na Mungu, na ni mwaminifu; kuliko niwe hapa na jina langu limeandikwa kwenye lile jengo, katika herufi za dhahabu namna hiyo, huku nikijua nimemwacha Mungu. Najua jambo hilo.” Hangenisikiliza tena, kwa hiyo akaingia ndani.

106 Lakini hivyo ndivyo ilivyo. Huwezi kumkatakata Mungu hata kidogo katika vipande viwili ama vitatu, vinavyoitwa “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” na kufanya Miungu watatu na kumpa Myahudi. Amri Yake yenyewe hasa ni, “Usiwe na miungu mingine mbele Zangu. Mimi ni Bwana Mungu wako.”

Yesu alisema nini?, Yesu alisema, “Sikilizeni, Enyi Israeli, Mimi ni Bwana Mungu wenu, Mungu mmoja.” Si watatu; hutawapa hao kitu hicho hata kidogo. La. Hakuna nabii wakati wo wote atakayehubiri juu ya Miungu watatu. La. Hakuna mahali po pote. Hutasikia jambo hilo kamwe. La, bwana. Huo ni upagani na ukafiri tu kama huko unakotokea. Ndiyo, bwana.

<sup>107</sup> Angalia. Lakini manabii hawa watakuja. Si hilo tu. . . Ma—manabii, sasa, ni Ufunuo 11. Tumesoma baadhi yake. Nami nawatakeni mlisome mnapojifunza kwa undani, kwenye kanda na kadhalika. Hao ni manabii waliothibitishwa kabisa, kwa ishara ya manabii. Ndipo Israeli watawasikia hao.

<sup>108</sup> Sasa, kwenu ninyi, marafiki zangu Mashahidi wa Yehova, fahamuni sasa ya kwamba hawa, mia na arobaini na nne elfu, hawana uhusiano wo wote na Bibi-arusi. Hakuna fungu hata moja la Maandiko linalounga jambo hilo mkono. La, bwana. Hao sio. Wao ni Wayahudi. Wale wateule walioitwa watoke katika wakati wa ile miaka mitatu na nusu ya majuma sabini ya Danieli. Sasa hiyo ni. . .

<sup>109</sup> Ni—ninanukuuu jambo hili mara kwa mara kila wakati. Sana sana si kwa ajili yenu ninyi nyote hapa, lakini, unaona, watu, hizi kanda huenda kila mahali, unaona. Na mnafahamu jambo hilo. Mnanisikia nikirudia kunukuu. Ni kwa kusudi hilo.

<sup>110</sup> Angalieni. Sasa angalieni jinsi wao walivyopaswa kuninii, vipofu, mnaona jinsi walipaswa. . . Yesu, ama. . . Ilibidi Mungu awapofushe Wayahudi, wasije wakamtambua Yesu. Laiti wanalijua, laiti tu wanalijua ya kwamba huyo. . . Kuona ishara aliyofanya Yeye, kama wanalikuwa katika hatua yao ya kweli, kama walivyokuwa huko zamani chini ya torati wakati Mungu alipowapa maelezo kuhusu nabii, nao walikuwa wamemwona Yesu akifanya hayo, wangelisema, “Huyu ndiye Masihi.” Kwa nini ilikuwa hivyo?

<sup>111</sup> Wale waliokuwa katika wakati ule, ambao majina yao yalikuwa yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, mitume Wake na kadhalika, waliona jambo hilo na kulitambua.

<sup>112</sup> Kwa nini hao wengine hawakuliona na kulitambua? Unaona, walikuwa wamepofushwa. Hawakuweza kuona jambo hilo. Hawalioni, hata hivi sasa. Wala hawataliona mpaka watakapozaliwa kama taifa, wakati mmoja. Hiyo. . .

<sup>113</sup> Neno haliwezi kukosea. Kumbukeni, Neno haliwezi kukosea. Sijali una miamsho mingapi, na kila namna ya mambo yanayotukia, hata hivyo Neno hilo haliwezi kukosea. Litakuwa jinsi vile hasa Mungu alivyosema lilikuwa. Unaona? Sasa, tunatambua ya kwamba mambo haya hayana budi kutukia.

<sup>114</sup> Na hiyo ndiyo sababu wao hawakumtambua Yesu wakati alipojitambulisha Mwenyewe kikamilifu kuwa ndiye Nabii yule.



115 Hata ma—maskini yule mwanamke mchafu Msamaria akisimama mahali pale kule kisimani. Yeye hajapata kufika huko Samaria; alienda tu kule, akasema alikuwa na haja ya kwenda kule, ndipo akaenda kule. Na kulikuwako na maskini mwanamke yule. Naye, katika hali yake, yeye alikuwa katika hali nzuri zaidi ya kupokea Injili kuliko wale makasisi wa kidini na watu wengine wa zama hizo. Aliipokea. Kweli. Sasa, unaona?

116 Lakini, mbele ya kukataa kwao kote, hata hivyo mmoja wa watu wao walio waungwana sana alikubali ya kwamba wao walijua alikuwa mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu.

117 Nilikuwa nikizungumza na mmoja wa madaktari walio bora sana walio katika majimbo ya kusini, ofisi kwake, si muda mrefu uliopita. Bingwa maarufu sana huko Louisville, mtu hodari sana. Nami nikamwambia, nikasema, “Daktari, nataka kukuuliza swali.”

Akasema, “Sawa.”

118 Nikasema, “Niliona nembo yenu ya utabibu, ile fimbo. Mna nyoka aliyenyongwanyongwa kwenye mti. Hiyo inawakilisha nini?”

Akasema, “Sijui.”

119 Ndipo nikasema, “Inawakilisha jambo hili: ilikuwa ni ishara ya uponyaji wa Kiungu, pale ambapo Musa alimwinua yule nyoka wa shaba kule jangwani, unaona, ambao ilikuwa ni mfano tu, ni mfano tu wa Kristo wa kweli.”

120 Sasa, leo, dawa ni ishara ya uponyaji wa Kiungu. Na ingawa wengi wao hawaamini jambo hilo, madaktari wazuri wa kweli wanaamini hilo. Lakini wengine wao hawaamini. Lakini nembo ile ile wanayoshikilia inashuhudia Nguvu za Mwenyezi Mungu, watake kuamini wasitake. Unaona? Hiyo ni kweli. Huyu hapo nyoka wa shaba amening’inia mtini, kwenye ile nembo ya utabibu.

121 Sasa waangalie hawa Wayahudi. Sasa, magamba ya upofu yalikuwa kwenye macho ya watu hawa. Wao, walilazimika kufanya hivyo; yalikuwapo, na Mungu aliyaweka hapo. Na yangali yapo hapo mpaka wakati ambao wao wameahidiwa, manabii hawa wajao. Mnaweza kupeleka wamishenari, mnaweza kufanya lo lote mtakalo; Israeli haitaongolewa mpaka hawa manabii watakapojitokeza, na hiyo itakuwa ni baada ya Kunyakuliwa kwa Kanisa la Mmataifa.

122 Wala wakati wa ndama haungeweza kupokea wito wa simba, kwa maana Mungu amesema katika Neno Lake, ya kwamba Roho wa ndama alitoka. Na katika ule wakati wa watengenezaji, mwanadamu alitoka. Unaona? Unanini tu. . .

123 Hilo ndilo jambo pekee wewe. . . wanaloweza kupokea. Hilo ni. . . Na, humo ndani sasa, wao wamepofushwa. Hivyo ndivyo ilivyo. Sasa angalia.

124 Lakini wakati waja ambapo Mataifa yataachwa. Kuna mti, na mizizi yake ilikuwa ya Kiyahudi, nao ulikatiliwa mbali; na Mmataifa akapandikizwa, “mzeituni, mwitu,” na unazaa tunda lake. Sasa, wakati Bibi-arusi huyo Mmataifa atakapokatiliwa mbali, huo mti wa Bibi-arusi nilionena habari zake, na utwaliwe upelekwe katika Uwepo wa Mungu; Mungu atawafutilia mbali hao Mataifa wasioamini, kando upande huu (yule mwanamwali aliyelala), na kupandikiza tena. Aliahidi kufanya jambo hilo.

125 Na mpaka wakati huo, unapaswa tu kujua ambapo... Kama unajua unakoelekea, vema, sawa. Kama hujui, mbona, unajikwaa gizani.

126 Sasa, hapo ndipo Wayahudi watakapoongolewa, katika wakati huo. Sasa, kama vile wakati wa kanisa, chini ya nguvu ya ahadi iliyotiwa upako, watampokea Kristo; lakini, sasa, si wakati Mataifa wako ndani. Sasa tunaweza kuona ni ujumbe wa aina gani ambao manabii hawa wawili, wa Ufunuo mlango wa 11, watahubiri. Sasa mnaweza kuona dhahiri kabisa jambo watakaloenda kufanya. Kwa kuwa, hao waliosalia, ama wale mia na arobaini na nne elfu, waliochaguliwa tangu zamani, watakapokea Muhuri wa Mungu.

127 Hebu na tusome tu. Sasa sikilizeni kwa makini sana sasa. Sasa nataka msome pamoja nami, kama mkiweza, kwa maana nitarejea kwenye jambo hili katika muda mfupi tu. Sura ya 7, sasa, hii ni kati ya Muhuri wa Sita na wa Saba.

*Baada ya haya—baada ya haya (Mihuri hii) . . .*

128 Ule Muhuri wa Sita ulifunguliwa, na huo ni wakati wa ile Dhiki. Kila mtu anafahamu jambo hilo sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Muhuri wa Sita ulifunguliwa, ndipo ile Dhiki ikaanza. Baada ya haya, yapi?

*Baada ya hayo nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne za nchi, upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote. (Malaika wanne!)*

*Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka maawio ya jua, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai; akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru bahari, nchi . . . bahari,*

*Akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, mpaka tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa . . .*

129 Si Bibi-arusi. “Watumishi.” Si wana. “Watumishi.” Israeli daima wamekuwa ni watumishi wa Mungu. Kanisa ni wana, unaona, kwa kuzaliwa. Israeli ni mtumishi Wake. Angalia, kila mahali, ndivyo ilivyo daima. Ibrahimu alikuwa ni mtumishi Wake. Sisi si watumishi. Sisi ni wana, wana na mabinti. Naam.

*. . . wa . . . wa Mungu wetu juu ya kipaji cha uso wao.*

130 Sasa angalia.

*. . . Mungu wetu katika kipaji vya nyuso zao.*

*Nikasikia hesabu yao waliotiwa muhuri. . .*

131 Sasa nawatakeni msikilize kwa makini kusomwa kwao.

*. . . hesabu yao waliotiwa muhuri katika kila kabila ya Waisraeli, watu mia na arobaini na nne elfu.*

132 Yeye anawataja kikamilifu. Sasa, kama ikitukia kwamba kuna Mwingereza-Mwisraeli mtambuzi anayeketi hapa, sikiliza vile jambo hili linavyolisahihisha jambo hilo, unaona.

*Wa kabila a Yuda kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. (Wanaitwa, “kabila.”) Wa kabila ya Reubeni kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Gadi. . . kumi na mbili elfu.*

133 Angalia ninii yako—angalia makabila yako sasa.

*Na wa kabila ya Asheri kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. . . kabila na Naftali kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. . . kabila ya—ya Manase. . . kumi na mbili elfu.*

*Na Kabila ya Simeoni. . . kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. . . Wa Kabila ya—ya Lawi kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Isakari kumi na mbili elfu. (Isakari, nafikiri ndivyo mnavyolitamka hilo). . . kumi na mbili elfu.*

*. . . kabila ya Zabuloni kumi. . . na mbili elfu. Na wa kabila ya Yusufu kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa nanii lote. . . Wa kabila ya Benyamini kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*

134 Sasa, hayo hapo yale makabila kumi na mawili, elfu kumi na mbili kutoka katika kila kabila. Kumi na mbili mara kumi na mbili. . . ni ngapi? [Kusanyiko linasema, “Mia na arobaini na nne elfu.”—Mh.] Mia na arobaini na nne elfu. Sasa angalia. Hao walikuwa, wote, wa makabila ya Israeli.

135 Sasa angalia, “Baada ya haya. . .” Sasa hapa linakuja kundi lingine. Sasa, Bibi-arusi ameondoka, tunajua jambo hilo. Lakini angalia kundi hili likija.

*Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, . . . kabila, jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mkononi mwao;*

*Wakalia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo.*

*Na mataifa. . . wote walikuwa wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi, na za huyo mzee, na za wale*

*wenye uhai wanne, nao wakaanguka kifulifuli mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu,*

*Wakisema, Amina; Baraka . . . utukufu . . . hekima . . . shukrani . . . heshima . . . uweza . . . nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.*

*Na mmoja wa wale wazee . . .*

136 Sasa yeye yuko mbele ya wazee hapa. Kwa kuwa, tumemwona yeye, wakati wote katika ile Mihuri.

*Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je! watu hawa . . .*

137 Sasa, Yohana, akiwa Myahudi, aliwatambua watu wake mwenyewe. Yeye aliwaona katika utaratibu wa kikabila. Hiyo ni kweli? Yeye aliwatambua na kuita kila moja la hayo makabila.

138 Lakini sasa, wakati anapowaona hawa, yeye kwa namna fulani anatatzwa. Na huyo mzee anajua jambo hilo, kwa hiyo anasema:

*. . . Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? nao wametoka wapi?*

139 Yohana, akijibu sasa:

*Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe.*

140 Yohana hakuwajua, unaona; jamaa wote, na lugha, na taifa.

*. . . Akaniambia, Hao ndio . . .*

*Akaniambia, hao ndio wanaotoka katika dhiki ile iliyo kuu, (kwa maneno mengine, ile Dhiki iliyo kuu), nao wamefua mavazi yao, . . . kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.*

*Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na wao . . . yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao.*

*Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote.*

*Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.*

141 Sasa tunafungua ile..tuuendee ule Muhuri.

Je! mlitambua, wao walikuwa . . .Kwanza, tunaanza sasa, Israeli.

142 Na basi tunaona kanisa lililotakaswa, si Bibi-arusi; kanisa lililotakaswa, kwa Dhiki, unaona, unaona, likija hapa, kundi kubwa la watu walio na mioyo minyofu hasa waliotoka kwenye—kwenye ile Dhiki kuu. Si Kanisa; Hilo limeshaenda, yule Bibi-arusi. Hilo hapo kanisa.

143 Sasa tunaona ya kwamba, baadaye kidogo, Yesu alisema ya kwamba kile Kiti cha Enzi kingewekwa, na jinsi ninii. . . wao wangesimama hukumuni, kila mmoja.

144 Sasa, tunaona sasa ya kwamba watu hawa walitiwa muhuri kwa Muhuri wa Mungu aliye hai (hiyo ni kweli?), hawa Wayahudi. Muhuri wa Mungu aliye hai ni nini?

145 Sasa, simwiti ye yote, simuudhi ye yote. Ninasema tu, unaona. Je! mnajua, ya kwamba, mkisoma wanachuo wengi wanaoandika juu ya hili, wanadai ya kwamba kundi hili hapa, lililoosha kwa damu, kwa kweli ni Bibi-arusi?

146 Je! mljua ya kwamba wanachuo wengi pia wanadai ya kwamba wale mia na arobaini na nne elfu ni Bibi-arusi? Ni ninii. . . Kuna kitu fulani hakina budi kuingia hapa, vibaya. . . ndani hapa vizuri, kwa sababu kuna kasoro fulani sasa.

147 Angalia, ndugu zetu Wasabato wanasema, ya kwamba, “Muhuri wa Mungu, ni kushika siku ya sabato.” Mnajua jambo hilo. Lakini ninataka kipengele kimoja kidogo sana cha Maandiko juu ya jambo hilo, kuonyesha ya kwamba sabato, ama kushika siku ya sabato, ni Muhuri wa Mungu. Unaona? Ni mtu fulani tu aliyetoa wazo hilo.

148 Lakini kama utasoma Waefeso 4:30, inasema, “Msimhuzunisha yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ninyi. . . ya ukombozi wenu,” naam, bwana, wakati kazi ya upatanisho imekwisha, nanyi mmekuja; Kristo anakuja kuwakomboa walio Wake. Mmetiwa Muhuri; si mpaka ufufuo mwingine. Ukiisha kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu, ni kazi iliyomalizika, ya kwamba Mungu amekupokea, wala hakuna kuepuka jambo hilo.

149 Unasema, “Vema, nilimpokea, halafu nikatoka.” La, hu—hukumpata.

150 Mungu alisema inaendelea hata Siku ya Ukombozi. Sasa, aha, wewe sasa bishana na Yeye, uone yale inayomaanisha. “Hata Siku ya Ukombozi wako.”

151 Angalia. Kadiri walivyokuwa. . . Kadiri walivyokuwa ni mabaki kulingana na uteuzi, hawa Wayahudi sasa ni mabaki kulingana na uteuzi. Katika siku za huduma ya kwanza ya Eliya kwa Wayahudi, ambapo waamini elfu saba walihifadhiwa kwa mkono wa Mungu, sasa kuna katika wakati huu wa mabaki, wakija kwenye wakati wao, kutimia mia na arobaini na nne elfu kulingana na uteule. Kwamba, Ujumbe wakati huo, kuamini Ujumbe huo, itakuwa ni wale mia na arobaini na nne elfu.

152 Sasa, unasema, “Loo! sasa ngoja kidogo, ndugu, mimi sijui habari za mambo haya ya “uteule.” Vema, kamwe sikuusoma pale.”

153 Vema, sasa hebu na tuone kama ni kweli, ama si kweli. Hebu na tufungue nyuma kwenye Mathayo, na twende chini hapa na

tuone kama hatuwezi kupata kitu fulani kidogo juu ya jambo hili mahali fulani. Ninaamini sasa ya kwamba mimi niko sahihi. Sijaliandika hapa chini, lakini ndiyo kwanza liingie moyoni mwangu. Hebu na tuchukue, mwishoni, aya ya 30; mahali tulipoenda jana usiku, kule kumalizia kwa ule Muhuri wa Sita, kwenye aya ya 30. Sasa hebu na tusome hiyo na tuone sasa mahali tunapofikia, aya ya 31. Unaona? “Watamwona Mwana wa Adamu akija katika utukufu.” Sasa aya ya 31.

*Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu.*

154 “Wateule” watatoka. Ni kitu gani? Na ule wakati wa ile Dhiki. Mungu atawaita wateule Wake, na hao ni Wayahudi katika wakati huo, wateule. Biblia inanena habari zake. Paulo ananena habari zake, “Kka uteule.” Kutakuwako na mia na arobaini na nne elfu kka uteule, ambao wataupokea Ujumbe, kutoka katika mamilioni watakaokuwa kule.

155 Kulikuwako na mamilioni katika Palestina, katika siku za unabii wa Eliya, na elfu saba waliokolewa kutoka katika mamilioni.

156 Sasa, “kka uteule.” Ambapo, mamilioni ya Wayahudi wanakusanyika katika nchi ya uenyeji wao. Limekuwa taifa. Kutakuwako na mamilioni mle, lakini ni mia na arobaini na nne elfu ya “wateule” tu watakaotwaliwa. Hao watausikia Ujumbe.

157 Ni jambo lile lile katika Kanisa la Mataifa. Kuna Bibi-arusi, naye ameteuliwa. “Naye ataitwa kulingana na uteule.” Angalia, hili lote linaonyesha mfano wa Kanisa, kikamilifu, waamini walioteuliwa.

158 Wengine hawaamini. Unaweza tu kujua jambo hilo. Unamwambia mtu Kweli, na ngoja ihakikishwe kwa Neno, na halafu ithibitishwe; yeye atasema, “Siamini jambo Hilo.” Unaweza tu kuninii . . .

159 Usijipumbaze na jambo hilo tena. Yesu alisema usijipumbaze. Alisema, “Ni kama tu kutupa lulu mbele ya nguruwe mwitu.” Unaona? Kasema, “Waacheni tu. Watageuka na kukukanyaga chini ya miguu yao. Wao watakudhihaki. Ondoka tu uwaache. “Kipofu akimwongoza kipofu . . .”

160 Nilienda kwa mtu mmoja, si muda mrefu uliopita; alinjia, hasa. Alikuwa akibishana, hapa na pale, kila mahali, akipinga uponyaji wa Kiungu. Naye akaja, na akasema, “Siamini uponyaji wako wa Kiungu.”

161 Nikasema, “Wangu, ninaamini, hautafaa kitu, maana sina wo wote.” Naye . . . Nikasema, “Lakini wa Mungu ni mkamilifu.”

Akasema, “Hakuna kitu kama hicho.”

162 Nikasema, “Umechelewa sana kusema jambo hilo, rafiki. Naam, ume—umengojea muda mrefu sana kufanya jambo hilo. Ungaliweza kubishana, miaka michache iliyopita, lakini huu ni wakati mwingine sasa. Kuna mamilioni wanaoweza kulishuhudia hili, unaona.” Nikasema, “U—umechelewa sana sasa, rafiki, kusema jambo hilo.”

163 Akasema, akasema, “Vema, siamini jambo hilo; sijali utafanya nini.”

Nikasema, “Hasha. Huwezi.” Unaona?

164 Akasema, “Nipige kwa upofu!” Kasema, “Kama kweli una Roho Mtakatifu, kama Paulo,” kasema, “nipige kwa upofu.”

165 Nikasema, “Nawezaje kufanya jambo hilo wakati wewe tayari ni kipofu?” Nikasema, “Baba yako amekupofusha usiione ile Kweli.” Nikasema, “Wewe, wewe ni kipofu tayari.”

166 Naye akasema, “Nisingeamini; Sijali yale ungeweza kufanya, ushuhuda mkuu vipi unaoweza kuthibitisha, au kitu cho chote kama hicho. Bado siamini.”

167 Nikasema, “Bila shaka. Haikuwa kwa ajili ya wasioamini. Ilikuwa kwa ajili ya waamini peke yao. Naam.” Unaona?

168 Ilikuwa ni kitu gani? Unaona, unajua papo hapo, uteule hauko. Usijipumbaze nalo kamwe, hata kidogo. Yesu alifanya jambo lile lile. Alisema, “Waacheni. Kipofu akimwongoza kipofu mwenziwe, si wataanguka wote shimoni?”

169 Lakini alipomjia maskini kahaba mdogo, [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] ilishika moto! Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni mbegu iliyoteuliwa iliyokuwa pale, unaona, iliyoliona Hilo sasa hivi. Wakati Hilo lilipomjia Petro, kulikuwako na mbegu iliyoteuliwa imekaa pale, unaona, nao wakaliona. “Na wote alionipa Baba, alio-,” (wakati uliopita)—“nipa Mimi, watakuja. Watakuja Kwangu.” Loo, jamani! Ninapenda jambo hilo! Naam, bwana. Angalia, waamini wanaamini jambo Hilo.

170 Wale wasioamini hawawezi kuamini Hilo. Kwa hiyo, sasa, kama mtu ye yote anataka kubishana juu ya uzao wa nyoka na kadhalika, nawe unajaribu kuwaonyesha, hawatasikiliza Hilo; ondoka tu uende zako. Waacheni tu. Unaona, Mungu habishani, wala watoto Wake.

171 Angalia, wale Wayahudi mia na arobaini na nne elfu walioteuliwa na Mungu hawamsujudu yule mnyama, na umadhehebu wake, wala sanamu zake, wala cho chote kile, ingawa taifa lao limefanya agano naye wakati huo. Israeli wako katika agano, lakini hapa kuna wale mia na arobaini na nne elfu ambao hawatafanya jambo hilo. Hao ni wale wateule.

172 Jambo lile lile ndivyo ilivyo hapa katika Kanisa la Mataifa sasa, ni kundi lililoteuliwa. Huwezi kuwaingiza katika upuuzi wa namna hiyo. Hawatauamini. La, bwana. Wakati ile Nuru

ilipowashukia tu, hilo linatosha papo hapo. Wao wanaona ninii. . . wanaona likitukia, halafu wanaliona likithibitishwa na kuhakikishwa namna hiyo. Kisha wanaangalia hapa katika Biblia, wanaona hilo Neno likiendelea tu. Vema, afadhali tu—afadhali uache kujipumbaza nao, maana wao wanaliadini Hilo. Ni hilo basi. Ni hilo tu basi. Ingawa hawawezi kulieleza jambo Hilo, lakini wao wanajua wamelipata. Kwa hiyo, kama ninavyosema, kuna mambo mengi sana siwezi kuyaelezea, lakini na—najua ni halisi hata hivyo. A-ha. Vema.

<sup>173</sup> Wakati huu ulikuwa kati ya ule Muhuri wa Sita na wa Saba, ambapo Yeye anawaita watu hawa, walionenwa na Yesu katika Mathayo sura ya 24 na aya ya 31, ambayo ndiyo sasa hivi tu tumeisoma, unaona. Parapanda hapa, wale mashahidi wawili wa. . . Wakati baragumu inapolia, ni parapanda ya wale mashahidi wawili wa wakati wa neema kwa Wayahudi. Parapanda moja inalia, unaona, baragumu moja inalia. Yeye alisema, “Na kupiga parapanda.” Sasa angalia hapa, ya 31.

*Naye atawatuma malaika zake* (si mmoja, unaona; wako wawili) pamoja *na sauti kuu ya parapanda*, . . .

<sup>174</sup> Ni kitu gani? Wakati Mungu anapokaribia kunena, kuna sauti ya parapanda. Hiyo sikuzote ni Sauti Yake. Ni kuita kwenda vitani, unaona. Mungu ananena. Malaika hawa watatokea na sauti ya baragumu.

<sup>175</sup> Nawe unaona, kwenye Ujumbe wa yule malaika wa mwisho, baragumu inalia. Ujumbe wa malaika wa kwanza, baragumu inalia; wa malaika wa pili, baragumu ililia, wakati Yeye alipoutuma. Angalia, lakini wakati ile Mihuri ilipotangazwa, yote ilikuwa katika jambo moja kuu la Kiungu, kuliita kundi fulani la watu litoke; kulitokea sauti moja ya baragumu, na Mihuri Saba ikavunjwa.

<sup>176</sup> Angalia, “Kuwakusanya wateule Wake kutoka sehemu nne za mbinguni.”

<sup>177</sup> Yeye alitaja Mihuri sita, kama tulivyoona, lakini si ule Muhuri wa Saba. Yeye hajasema jambo lo lote hapa kuhusu Muhuri wa Saba, hata mahali pamoja.

<sup>178</sup> Unaona, mara moja, kifungu cha 32, kinageukia mifano, ya wakati wa kule kuitwa kwa wale Wayahudi walioteuliwa. Sasa angalia hapa, unaona.

<sup>179</sup> “Naye atawatuma malaika pamoja na baragumu, na kuwakusanya wateule kutoka pembe nne za mbinguni.” Sasa anaanza. . .

<sup>180</sup> Unaona, Yeye hasemi neno juu ya Muhuri wa Saba hapa. Unaona? Alinena juu wa Muhuri wa Sita; wa Kwanza, wa Pili, wa Tatu, wa Nne, wa Tano, na wa Sita.

<sup>181</sup> Lakini angalia:



*Basi kwa mtini jifunzeni mfano; matawi yake yakiiisha kuchipuka na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu;*

*Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni.*

182 Hilo la mwisho, hilo swali walilomuuliza, “Na ni nini dalili ya mwisho wa ulimwengu?”

183 “Wakati mtakapowaona hawa Wayahudi... Mtakapoona mambo haya mengine yakitukia, mnajua yale yanayotukia. Sasa, mtakapoona hawa Wayahudi...” Akiwazunguzia Wayahudi! Sasa angalia. Yeye anazungumza na kundi gani, Mataifa? Wayahudi! Wayahudi! Unaona?

184 Sasa Yeye alisema, “Mtachukiwa na mataifa yote kwa ajili ya Jina Langu,” na kadhalika, vivyo hivyo.

185 Sasa, “Wakati,” Yeye alisema, “mtakapoona hawa Wayahudi wakianza kuchipusha na kuchanua majani yao kule,” wakati hao Israeli watakapoanza kugeuka, kurudi nchini mwao. Wakati watakapofika kule, (Kanisa liko tayari kwa Kunyakuliwa), kuna miaka mitatu tu na nusu iliyosalia mpaka kufikia mwisho wa ulimwengu wa kale, halafu unaingia katika machafuko, ndipo ule Utawala wa Miaka Elfua unaingia, kwenye mpya—nchi mpya. Kasema, “Uko mlangoni!” Sasa, miaka elfu moja duniani ni siku moja tu kwa Mungu. Na miaka mitatu na nusu, ingekuwa ni siku ngapi? Sekunde kadha, katika wakati wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Uko mlangoni.”

*Amin, nawaambia, ya kwamba, Kizazi hiki hakitalimizika, hakitapita, watu hawa, mpaka hayo yote yame-...*

186 Ni, ni kitu gani hakitapita? Wao wamejaribu kuwauwa Wayahudi, kuwaangamiza duniani, daima. Hawataweza kufanya jambo hilo kamwe.

187 Lakini angalia. Kizazi kile kile cha Wayahudi kilichoona kule kurudi, kurudi katika Palestina, kizazi hicho kingeona mambo haya yakitukia. Na kwa miaka miwili tu iliyopita, limekuwa taifa kamili, likiwa na pesa zake lenyewe na cho chote kile. Hilo hapo.

188 Sasa sisi tuko wapi, ewe rafiki? Mihuri na kila kitu vikifunguliwa; sasa tunapata jambo hili katikati hapa. Hilo hapo. Unaona mahali tunapoketi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

189 Natumaini mnalipata Hilo. Sina elimu yo yote. Ninajua ninalozungumzia, lakini labda siwezi kulieleza—kulieleza, kulifanya dhahiri kwenu. Lakini ninatumaini ya kwamba Mungu atachukua maneno ambayo yamechanganyikana, na kuyagawanya vizuri, unaona, na kuwafanya mjue ni Kitu gani.

Maana, ni, tuko mlangoni. Tuko hapa kwenye ule wakati. Sasa angalia.

<sup>190</sup> Unaona, mara moja sasa, Yeye anawageukia hawa Wayahudi, na kwenye ninii—kwenye wakati wa mwisho. Yeye anasema jambo litakalotukia. Tunajua hata sasa jambo hilo sasa ni niiii. . . Tunajua, tunafahamu vyema kabisa, ya kwamba yale makabila yametawanywa. Yamekuwa hivyo, kwa miaka elfu mbili na mia tano. Yalitabiriwa yatatawanyika kwenye pepo nne. Mlijua jambo hilo? Tunajua hivyo.

<sup>191</sup> Bila shaka, haitatulazimu kurudi nyuma na kupata, kuchukua hilo, maana nina jambo fulani hapa lililo muhimu sana ninalotaka mwone, kabla hamjachoka sana, nami nichoke.

<sup>192</sup> Angalieni. Tunajua, hata kila kabila, huo ni utaratibu wa miaka wa kikabila, ama vyo vyote unavyotaka kuuita, ama jiolojia, ama mahali pa kikabila, hawako pamoja tena. Wametawanyika, kila mahali.

<sup>193</sup> Wayahudi, wanakusanyika Yerusalemu, si. . . Hata hawajui makabila yao. Hawana tena bendera za kikabila wala cho chote kile. Yote wajuayo, basi, ni kwamba wao ni Wayahudi. Walitabiriwa kuwa namna hiyo, kila mahali ulimwenguni. Sasa, vitabu vyao vimeteketezwa. Huwajui.

Unasema, “Wewe ni wa kabila gani?”

“Sijui.”

“Kabila gani?”

“Sijui.”

<sup>194</sup> Mmoja kutoka Benyamini, mmoja kutoka *hili*, na mmoja kutoka *lile*. Hawajui wametoka kwa lipi. Vitabu vyao vimeteketezwa, katika vita, na kwa miaka elfu mbili na mia tano. Jambo pekee wajualo, wao ni Wayahudi. Hilo tu. Kwa hiyo, wao wanajua wamerudi katika nchi ya uenyeji wao. Wao bado. . . Angalia, ingawa hawajui makabila yao, bali Mungu anajua.

<sup>195</sup> Ninapenda tu jambo hilo! Unajua, Yeye hata alisema kuna. . . “Kila unywele wa kichwa chako umehesabiwa.” A-ha! Angalia, Yeye hapotezi cho chote. “Nitakizifufua tena katika siku ya mwisho.”

<sup>196</sup> Ingawa wamepoteza bendera zao—zao—zao za kikabila, na yupi ni *nani*, na kama wao ni *hili* ama *lile*; wao hawajui kama wametoka kwa Benyamini, ama kama wametoka kwa Reubeni, ama—ama Isakari, ama wametoka katika kabila lipi. Lakini, hata hivyo, Mungu anawaita hapa.

<sup>197</sup> Sasa angalia, katika Ufunuo 7, tunasoma hivi. “Kumi na mbili elfu” wa kila kabila, walioteuliwa, kutoka kwa hao wote. Kuna kumi na mbili elfu kutoka katika kila kabila, walioteuliwa, nao wameketi papa hapa katika utaratibu. Loo! jamani! Wao

ni akina nani? Wao wako katika utaratibu wa kikabila. Hata hivyo, wao sivyo walivyo sasa, bali watakuwa hivyo. Wako katika uratatibu wa kikabila. Ni akina nani watakaokuwa katika utaratibu wa kikabila? Si Myahudi wa kawaida, la. Bali wale walioteuliwa, wale mia na arobaini na nne elfu, watawekwa katika utaratibu wa kikabila. Loo, jamani!

198 Jinsi ningetaka kuwaonyesha! Hatutaingilia jambo hilo. Lakini hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa, a-ha, moja kwa moja katika utaratibu.

199 Sasa nawatakeni mwangalie kwa makini sana na msome pamoja nami, kwa dakika moja. Sasa hapa kuna jambo ambalo labda hamkuona katika kule—kule kuitwa kwa makabila. Niliwaambia, muda mfupi uliopita, kusoma Ufunuo 7. Someni pamoja nami, na myaangalie makabila hayo. Katika Ufunuo 7, Dani na Efraimu hawamo wala hawajahasabiwa pamoja nao. Mliona jambo hilo? Yusufu na Lawi waliwekwa mahali pao. Mliona jambo hilo? Dani na Efraimu hawamo. La, bwana. Lakini, Yusufu na Lawi waliwekwa badala ya—ya—ya Dani na Efraimu.

200 Kwa nini? Wao . . . Mungu anayekumbuka daima hukumbuka kila ahadi ya Neno Lake. Loo! ningetaka kuhubiri juu ya jambo hilo. Unaona? Mungu hasahau kitu, hata ingawa inaonekana kama husahau.

201 Kama vile alivyomwambia Musa. Israeli walikuwako kule, “miaka mia nne.” Iliwabidi kwenda kule wakati huo. Yeye alimwambia Ibrahimu, “Na uzao wake ungekuwa mgeni katika nchi ya ugeni kwa muda wa miaka mia nne, kisha Yeye angewatoa kwa mkono wenye nguvu.” Lakini basi Yeye alimwambia Musa, “Nimekumbuka ahadi Yangu, nami nimeshuka kutimiza yale niliyosema.”

202 Mungu hasahau. Yeye hasahau laana Zake, wala hasahau baraka Zake. Lakini, kila ahadi ambayo Yeye alifanya, Yeye hudumu nayo.

203 Hii ndiyo sababu wao walikuwa hawako, sasa, kama ukiangalia. Sasa someni. Nawatakeni msome pamoja nami sasa. Fungueni katika Kumbukumbu la Torati aya ya ishiri- . . . aya ya 29 pale, ama mlango wa 29, hasa. Kuna sababu makabila haya kutokuwa pale. Kila kitu kina sababu yake. Kumbukumbu la Torati, tunataka kuchukua m—mlango wa 29 wa Kumbukumbu la Torati. Sasa, naomba Bwana atusaidie, ili kwamba tuweze kuelewa sasa. Sasa tunataka kuanzia katika Kumbukumbu la Torati, sura ya 29, kwenye aya ya 16. Sasa sikilizeni. Musa akinena.

*(Kwani mwajua tulivyoketi katika nchi ya Misri, na tulivyokuja katikati ya mataifa hayo tuliyoipita katikati yao;*

*Nanyi mliona machukizo yao, na sanamu zao, miti . . . mawe, fedha . . . dhahabu, zilizokuwako kwao;)*

204 Kila mmoja alibeba kitu fulani kidogo ama cho chote kile, kijisanamu kidogo cha Mtakatifu Cecilia. Unajua, kitu kama hicho, unaona. “Hivyo basi asiwe . . .” Sikilizeni.

*Asiwe mtu kati yenu, mume . . . mke, wala jamaa, wala kabila, ageukaye moyo wake leo amwache BWANA, Mungu wetu, kwenda kuitumikia miungu ya mataifa haya; lisiwe katikati yenu shina lizaalo uchungu na pakanga;*

*Ikawa asikiapo maneno ya laana hii, aji—ajibarikie mtu huyo moyoni mwake, na kusema, mimi . . . -takuwa katika amani, nijapotembea katika upotoe wa moyo wangu . . .*

205 Unaona, watu wanasema, “Loo! yeye anajibariki.” Unajua, anafanya alama ya msalaba mdogo ama cho chote kile, kama wanavyofanya siku hizi, unaona; jambo lile lile, unaona. Na mnaona ni tabia ya kikafiri, unaona, ka—kafiri.

*. . . yeye hujibariki moyoni mwake mwenyewe, . . . moyoni mwake mwenyewe katika nia yake, kuongeza ulevi kwenye kiu;*

206 “Kunywa tu, hilo halidhuru kitu; mradi tu unaenda kanisani, huna neno.”

*Basi BWANA hatamsamehe mtu huyo, lakini wakati huo hasira ya BWANA . . . wivu wake vitafuka moshi juu ya mtu yule, na laana yote iliyoandikwa katika kitabu hiki (“Usiondoe Neno moja Kwake, wala kuongeza neno moja Kwake,” unaona.) itamkalia juu yake, na BWANA atalifuta lake . . . atalifuta jina lake chini ya mbingu.*

207 Hiyo ni wakati angali hapa duniani, unaona, “chini ya mbingu.”

*BWANA atamtenga kwa uovu kutoka kwake, kutoka kabila zote za Israeli, kwa laana zote za agano lililoandikwa katika chuo hiki cha torati.*

208 Kwa hiyo, “Kama mtu ye yote ataitumikia sanamu, au kujiwekea sanamu, au kujibariki mwenyewe moyoni mwake, na kuzitumikia sanamu,” Mungu alisema, “mwanamume, mwanamke, jamaa, ama kabila, jina lake litafutwa kabisa, kutoka kati ya watu.” Sasa, hiyo ni kweli? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Jinsi ilivyo kweli!

209 Ibada ya sanamu ilifanya jambo lile lile kanisani, miaka mingi iliyopita, na inafanya hivyo leo. Nami naona . . . Angalia jinsi mpinga—Kristo alivyojaribu kupinga. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Ibilisi anajifananisha na huwaigiza—huwaigiza watakatifu wa Mungu?

210 Dha—dhambi ni nini? Ni jambo la kweli likipotoshwa. Uwongo ni nini? Ni ukweli ukigeuzwa vibaya. Uzinzi ni nini? Ni tendo sahihi, tendo halali, likitendwa vibaya. Mnaona?

211 Sasa, katika kujaribu kufanya jambo hili, “kufuta jina fulani,” je! miona katika ule wakati wa kanisa, mnyama yule yule anayetumikia sanamu za watu waliokufa, na kadhalika, alijaribu kulifuta Jina la Bwana Yesu Kristo, na kutoa vyeo kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Jambo lile lile, akiwa na laana ile ile nyuma yake, namna hiyo.

212 Dani na Efraimu ndivyo walivyofanya kabisa, chini ya unafiki wa Mfalme wa Israeli, laghai, Yeroboamu. Sasa, angalia, katika Wafalme wa Kwanza, mlango wa 12. Najua tunaninii. . . Hili, kwangu mimi, li—li—linaweka msingi wa yale tunayoweza kutegemea, yale tunayoona. Wafalme wa Kwanza, ninataka kwenda kwenye mlango wa 12, aya ya 25 paka ya 30.

*Ndipo Yeroboamu. . . Shekemu katika milima ya Efraimu, akakaa huko. akatoka huko akajenga Penueli.*

*Na basi Yeroboamu akasema katika mo—moyoni mwake, (Unaona, katika upotoe wa moyo wake), Basi ufalme utairudia nyumba ya Daudi.*

213 Yeye alikuwa anaogopa, unaona, maana hao watu huenda wakaondoka.

*Kama watu hawa wakipanda. . . kutoa dhabihu katika nyumba ya BWANA huko Yerusalemu, ndipo mioyo ya watu hawa itamrudia bwana wao, yaani Rehoboamu, mfalme wa Yuda; nao wataniua mimi, na kumrudia Rehoboamu—Rehoboamu, mfalme wa Yuda.*

*Kwa hiyo mfalme akafanya shauri, akafanyiza ng'ombe wawili wa dhahabu, akawaambia watu, Ni vigumu kwenu kupanda kwenda Yerusalemu; tazama, hii ndiyo miungu yenu, Enyi Israeli, iliyowapandisha kutoka nchi ya Misri.*

*Akamweka mmoja katika Betheli, na wa pili akamweka katika Dani.*

*Jambo hili likawa dhambi, maana watu walikwenda kuabudu mbele ya kila mmoja, hata huko Dani.*

214 Unaona, Efraimu kule Betheli, na Dani, nao wakaweka sanamu. Nao hawa wakaenda kuiabudu hii.

215 Na tuko hapa, moja kwa moja katika ule Utawala wa Miaka Elfu, karibu, na Mungu angali anakumbuka dhambi hiyo. Wao hata hawahesabiwi miongoni mwao. Jamani! Utukufu! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Hakika kama vile anavyokumbuka kila ahadi nzuri, Yeye hukumbuka kila uovu, pia. Kumbuka tu, wakati. . .

216 Hiyo ndiyo sababu ninaamini, marafiki, daima nimejaribu kusimama na hilo Neno, haidhuru lionekane si kitu cha kawaida namna gani.

217 Unaona, sasa, wao hawangewazia juu ya jambo hilo pale wakati huo. Hawakulifikiria wakati huo. Walifikiria, “Vema, wameepukana na jambo hilo.” Vema.

218 Lakini hawa hapa upande huu katika wakati huu wa ule Utawala wa Miaka Elfu wamekaa, wakati majina yao na makabila yao “yamefutuliwa mbali” kutoka mle, kwa maana wao walitumikia ibada za sanamu, ambazo Mungu alilaani.

219 Je! Yeye hakusema “alichukia” Wanikolai na yule Yezebeli? Kaeni mbali na hayo. Je! Yeye hakusema angewaua binti za Yezebeli kwa kifo cha “mauti,” ambacho ni kutengwa Milele kutoka kwenye Uwepo Wake? Usiyategeme, hata kidogo. Yakimbieni. Kwa hiyo, Mungu hukumbuka. Angalia.

220 Lakini mliona pale, yalikuwa “yafutwe”? Kwa nini? Chini ya Mbingu hapakuwapo na Dhabihu ya moja kwa moja ambayo ingeweza kumpa Roho Mtakatifu, kumfanya aone mambo haya. Lakini alifanya jambo hilo, hata hivyo, katika nia yake mwenyewe ya kichoyo.

221 Lakini, Ezekieli, katika ono lake, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, yeye anawaona tena katika utaratibu mkamilifu. Ezekieli, kama ulitaka kusoma jambo hilo. Liandike tu, nawe unaweza kulisoma, kuokoa wakati. Ezekieli 48:1 hadi 7, pia soma 23 hadi 29. Ezekieli aliona kila kabila katika utaratibu kabisa. Vema.

222 Na, pia, katika Ufunuo 14, Yohana aliwaona tena katika utaratibu wa kikabila, hiyo ni kweli, kila kabila mahali pake. Ni kitu gani kilichotukia?

223 Mnakumbuka, Yeye alisema, “Chini ya mbingu, ya kwamba jina lake lingefutwa katika mambo ya kabila.” Mradi tu alikuwa chini ya mbingu, halingekuwako tena. Na hawa mia na arobaini na nne elfu wako chini katika sehemu ya kabila, bado. Sawa. Lakini, unaona, wao walikuwa wamepofushwa. Wao walikuwa tu na dhabihu za ndama na mbuzi. Unaona? Sasa angalia, Yeye aliwafuta, “chini ya mbingu.”

224 Lakini Mmataifa, katika siku za Roho Mtakatifu, dhidi ya Hiyo; jina lako lilifutwa kabisa kutoka kwenye kile Kitabu cha Uzima, “na hungeweza kusamehewa kamwe, katika ulimwengu huu ama uliwengu ujao.” Hiyo ni kweli? Kwa hiyo hapo ndipo tunaposimama.

225 Israeli, chini ya mbuzi, kondoo, wao—wao walikuwa na nafasi. Mradi tu walikuwa hapa duniani, makabila yao yalikuwa yanakosekana. Hawangeweza kamwe kuhesabiwa. Sasa, wote... Wakati Yeye alipowaita, kule, hao mia na arobaini na nne elfu, wao hawakuweko. Hiyo ni kweli. Hata

hawahesabiwi humo. Na Yusufu na Lawi wamewekwa mahali pa Dani na Efraimu. Sasa unaweza kuangalia jambo hilo. Liko papo hapo, mbele zenu, unaona. Na hapa pana ahadi ya Mungu, nyuma zamani kule, mamia na mamia ya miaka kabla ya jambo hilo. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara kadha wa kadha—Mh.]

226 Sasa, ni kitu gani kilichotukia? Wao walitakaswa katika wakati wa ile Dhiki mbaya sana.

227 Sasa, kama Mungu ataenda kumtakasa huyo—huyo mwanamwali, ambaye alikuwa ni mwanamke mnyofu, lakini alishindwa tu kutia mafuta kwenye taa yake, Naye atamtakasa kwa mateso humo. Yeye anayaweka hayo makabila moja kwa moja humo, kwa ajili ya jambo lile lile, na anawatakaswa katika wakati wa ile Dhiki. Kwa sababu, ni—ni kutakaswa. Ni hukumu. Lakini, unaona, wao, baada . . . Na, angalia hapa, hapa wanakuja wale mia na arobaini na nne elfu, baada ya kule kutakaswa kwa Israeli. Na hapa anakuja pia yule mwanamwali aliyelala, anatokea, ametakaswa, na amevaa mavazi marefu meupe. Mnaona? Jinsi lilivyo kamilifu! Jinsi hilo lilivyo zuri!

228 Ni kama tu vile Yakobo, katika wakati wa taabu, unaona. Wao . . . Yakobo katika wakati wa taabu. Yeye alikuwa amefanya makosa. Lakini alipitia katika wakati wa utakaso kwa sababu alikuwa amemkosea ndugu yake, Esau. Unaona? Yeye alidanganya, kusudi aichukue haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Lakini yeye alipitia katika wakati wa utakaso kabla hajabadilishwa jina lake kutoka Yakobo akawa Israeli, ambalo ni mfano wa taratibu ya Mungu, umefananishwa na wa siku hizi.

229 Sasa, tutageukia sasa kwenye kifungu cha 8 cha ninii . . . ama kifungu cha 1, namaanisha, cha mlango wa 8; cha Ufunuo 8:1

230 Ninajua mmechoka. Lakini, sasa, jaribuni tu kusikiliza tu kwa dakika chache sasa. Na, Mungu wa Mbinguni atusaidie, ndilo ombi langu.

231 Hatuna budi kukumbuka ya kwamba Muhuri huu wa Saba ni mwisho wa wakati, wa mambo yote. Hiyo ni kweli. Mambo yaliyoandikwa katika kile Kitabu cha Mihuri Saba, kilichotiwa muhuri, cha mpango wa ukombozi tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, kila kipengele kinafikia mwisho wake. Ni mwisho; ni mwisho wa ulimwengu unaotaabika. Ni mwisho wa maumbile yanayotaabika. Ni mwisho wa kila kitu. Ndani mle, ni mwisho wa zile Baragumu. Ni mwisho wa vile Vitasa. Ni mwisho wa dunia. Ni ninii . . . Hata ni mwisho wa wakati.

232 Wakati unakwisha. Biblia ilisema hivyo. Mathayo, sura ya 7 . . . Namaanisha, Ufunuo, sura ya 7 . . . sura ya 10 na ninii . . . na aya ya 1 mpaka ya 7. Wakati unakwisha. Yule Malaika alisema, “Hapatakuwa na wakati baada ya haya,” wakati ile, katika siku zile za kutukia kwa jambo hili kuu.

233 Kila kitu kinamalizika, katika wakati huu, mwisho wa—wa . . .mwishoni mwa Muhuri huu wa Saba. Angalia. Ni mwisho wa wakati wa kanisa. Nininii—ni mwisho wa Muhuri wa Saba. Ni mwisho wa zile Baragumu. Ni mwisho wa vile Vitasa, na hata ni mwisho wa kule kuingizwa kwa ule Utawala wa Miaka Eflu. Haya ni katika ule Muhuri wa Saba.

234 Ni kama tu kurusha roketi hewani. Na hiyo roketi inalipuka *hapa*, halafu inapanda juu na kisha inalipuka tena. Inatoa nyota tano. Moja ya nyota hizo inalipuka na kupasua nyota tano kutoka kwake; halafu moja ya hizo nyota inalipuka na kuzima nyota tano kutoka kwake. Unaona, inatoweka.

235 Hivyo, ndivyo ulivyo, Muhuri wa Saba. Unamalizia tu wakati kwa ulimwengu. Unamalizia wakati kwa jambo *hili*. Unamalizia wakati kwa *lile*. Unamalizia wakati kwa *hili*. Unamalizia wakati. Kila kitu kiliishia tu kwenye Muhuri huo wa Saba.

236 Sasa, Yeye atafanyaje jambo hilo? Hilo ndilo hatujui. Sivyo? Hatujui.

237 Hata ni wakati wa mambo haya yote, na kule kuingizwa kwa ule Utawala wa Miaka Eflu.

238 Angalia, kule kuvunjwa kwa Muhuri huu kulikuwa ni kuuu sana, hivi kwamba, Mbingu ilinyamazishwa na jambo Hilo, “ikawa kimya, kwa muda wa nusu saa.” Sasa, ni jambo kuu! Ni kitu gani? Ilinyamazishwa, Mbingu. Hakuna kitu kilichosogea, kwa nusu saa.

239 Sasa, nusu saa huenda isiwe ndefu kama una wakati wa furaha sana. Lakini, katika wasiwasi wa kati ya mauti na Uzima, ilionekana kama kipindi cha Miaka Eflu. Lilikuwa ni jambo kuu sana!

Yesu kamwe hakuutaja. Hakuna mwingine aliyeutaja.

240 Yohana hata hakuweza kuandika habari Zake. La, yeye alikatazwa kuandikwa *hapa*. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake mara mbili—Mh.] Unaona, kuna ninii tu . . .ninii tu . . . Yeye hakuandika, lakini huu umenyamaza.

241 Na wale wazee ishirini na wanne waliosimama mbele za Mungu, Pale, wakipiga vinubi vyao; waliacha kupiga vinubi vyao.

Malaika walinyamaza kuimba kwao, huko Mbinguni.

242 Wazia! Wale Makerubi na Maserafi watakatifu, ambao Isaya aliwaona hekaluni, wakiwa na seti sita . . .ama seti tatu za mabawa. Tatu . . .Mawili yalifunika uso wake, na mawili yalifunika miguu yake, na kuruka. Na usiku na mchana, Wao wako mbele za Mungu, wakiimba, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi!” Na hata wakati walipotembea kuingia, ama walipoingia hekaluni, nguzo za hekalu zilitikisika, kwa—kwa uwepo wao.



243 Na hawa Maserafi watakatifu walinyamaza. Malaika waliacha kuimba. A-ha. Whiu! Wakiruka katika Uwepo wa Mungu, wakiimba, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,” Walinyamaza. Hakuna Malaika wanaoimba. Hakuna sifa. Ha—hakuna ibada ya madhabahuni. Hakuna, hakuna cho chote. Kulikuwako na kimya; kulinyamaza, kimya kitupu Mbinguni, kwa nusu saa.

244 Jeshi lote la mbinguni lilikuwa limenyamaza kwa nusu saa hii, wakati siri hii ya Muhuri wa Saba katika Kitabu cha Ukombozi ilipovunjwa ikawa wazi. Wazia jambo hilo. Lakini, imevunjwa. Mwana-Kondoo anaivunja. Unajua nini? Wao walishikwa na hofu ya kicho kwa ajili Yake, naamini. Hawakujua; ulikuwa ndio Huo hapo! Walisimama tu.

245 Kwa nini? Ni kitu gani? Sasa, hakuna hata mmoja wetu ajuaye. Lakini, nita—nitawaambia, katika ninii yangu—katika ufunuo wangu wa jambo Hilo.

246 Na, sasa, mimi sipendi kuwa mshupavu wa dini. Kama hivyo ndivyo nilivyo, sina habari nalo, unaona. Mimi. . . Mimi sishiriki mambo ya kijinga kama ya kiinimacho na mambo ya uongo.

247 Nimesema mambo fulani, huenda yalikuwa kwa namna fulani mageni kwa watu fulani. Lakini wakati Mungu anapotokea hapo, nyuma ya Jambo Hilo, na kulithibitisha jambo Hilo na kusema ni Kweli, basi hilo ni Neno la Mungu. Unaona? Huenda likaonekana ni la kigeni, namna hiyo. Unaona?

248 Na sasa, kwa hakika kama ninavyosimama hapa kwenye jukwaa hili usiku wa leo, nilikuwa na ufunuo uliofunua. Uko katika sehemu tatu. Ambapo nitawaambia, kwa msaada wa Mungu, juu ya sehemu Yake moja. Na halafu ninyi. . . Hebu na tuangalie jambo hilo, kwanza. Huu hapa huo ufunuo, kuanza yale ninayotaka kuwaambia, kwamba Huo ni nini. Kinachotukia, ni kwamba. . . Zile Ngurumo Saba ambazo alizisikia zikinguruma, na akakatazwa kuandika; hizo ndiyo ile siri, iliyo nyuma ya hizo Ngurumo Saba zinazonguruma mfululizo. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara kadha wa kadha—Mh.]

249 Sasa, kwa nini? Hebu na tuthibitisha jambo hilo. Kwa nini? Ni ile siri ambayo hakuna mtu ajuaye. Yohana alikatazwa kuandika juu Yake, hata—hata kuandika mfano Wake. Kwa nini? Hii ndiyo sababu hakukuwako na shu—shughuli zo zote Mbinguni: ingetoa hiyo siri. Mnaona jambo hilo sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

250 Kama ni kuu namna hiyo, haina budi kujumlishwa, kwa maana haina budi kutukia. Lakini wakati zile Ngurumo Saba. . .

251 Sasa angalia. Wakati wale Malaika saba walipokuja kupiga baragumu zao, kulikuwako na ngurumo moja. [Ndugu Branham anapiga mimbara mara moja—Mh.] Wakati

Israeli walipokusanyika, kulikuwako na baragumu. “Wakati hapatakuwa na wakati baada ya haya,” ile baragumu ya mwisho, ngurumo moja.

<sup>252</sup> Lakini hapa kuna Ngurumo Saba mfululizo, moja baada ya nyingine: moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, hiyo namba kamilifu. Ngurumo Saba mfululizo, zilitoa sauti, si . . . zikifanya tu—tu moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, mfululizo. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara saba—Mh.] Ndipo, Mbingu hazingeweza kuandika jambo Hilo. Mbingu haziwezi kujua juu ya jambo Hilo, hakuna jambo lingine lo lote, maana hakuna jambo linaloendelea. Ilikuwa ni wakati wa kupumzika. Ilikuwa ni kuu sana, mpaka, ikafichwa Malaika.

<sup>253</sup> Sasa, kwa nini? Kama Shetani angeipata, huenda akasababisha uharibifu mkubwa. Hicho hapo kitu kimoja ambacho yeye hajui. Sasa, yeye anaweza kufasiri lo lote analotaka, na kuiga kila namna ya kipawa, (natumaini mnajifunza), lakini hawezi kujua jambo Hili. Hata halijaandikwa katika Neno. Ni siri kabisa.

<sup>254</sup> Malaika, kila kitu, kilinyamaza. Kama wangalifanya msogeo mmoja, huenda ingetoa kitu fulani, kwa hiyo wao walinyamaza tu, wakaacha kupiga vinubi. Kila kitu kilinyamaza.

<sup>255</sup> Saba, nambari ya Mungu iliyo kamilifu. Saba, [Ndugu Branham anapiga-piga mimbara mara saba—Mh.] moja kwa moja tu mfululizo. Ngurumo Saba zililia mfululizo pamoja, kama kwamba zilikuwa zikiendelea herufi za kitu fulani. Angalia, katika wakati huo, Yohana alianza kuandika jambo Hilo. Yeye akasema, “Usiliandike Hilo.”

<sup>256</sup> Yesu hakunena habazi Zake. Yohana hakuweza kuliandika. Malaika hawajui cho chote kuhusu Hilo. Ni nini? Ni kile kitu ambacho, Yesu alisema, “Hata Malaika wa Mbinguni hawakujua” kitu juu Yake. Unaona? Unaona? Yeye hakujuu, Yeye Mwenyewe. Kasema, “Ni Mungu tu” angejua jambo Hilo.

<sup>257</sup> Lakini Yeye alituambia, wakati “tutakapoanza kuona ishara hizi zikitokea.” Sasa mnaelekea mahali fulani? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Vema. Angalia, “tukianza kuona ishara hizi zikitokea.” Unaona?

Kama Shetani angeweza kulipata Hilo . . .

<sup>258</sup> Kama ukitaka jambo fulani litukie . . . Sasa itakubidi uchukue Neno langu kwa ajili ya jambo hili. Kama ninapanga kufanya jambo fulani, ninajua ninajihadhari sana kumwambia mtu ye yote juu yake. Si kwamba mtu huyo angesema jambo hilo, lakini Shetani atalisikia. Unaona? Yeye hawezi kulipata, ndani ya moyo wangu pale, mradi tu Mungu amelifunga kwa Roho Mtakatifu, kwa hiyo hilo ni kati yangu na Mungu. Unaona? Yeye hajui kitu juu ya jambo hilo mpaka wewe uliseme, ndipo analisikia. Nami nimejaribu . . . Ninawaambia watu nitafanya kitu fulani, basi angalia Ibilisi akizuia kila hatua awezayo,

kunizuia kufika mahali pale, unaona, kusudi anitangulie pale. Lakini nikipata ufunuo kutoka kwa Mungu, wala nisiseme jambo lo lote juu yake, basi ni tofauti.

259 Kumbuka, Shetani atajaribu kuiga. Atajaribu kuiga kila kitu ambacho Kanisa litafanya. Amejaribu kufanya jambo hilo. Tunaona jambo hilo, kupitia kwa mpinga-Kristo.

260 Lakini hili ni jambo moja ambalo yeye hawezi kuiga. Hakutakuwako na kuiga kwa jambo hili, unaona, maana yeye hajui jambo Hilo. Hawezi kulijua kamwe. Ni ule Mvuto wa Tatu. Yeye hajui kitu kabisa juu Yake. Unaona? Yeye haufahamu.

261 Lakini kuna siri iliyo chini ya jambo Hilo! [Ndugu Branham anapiga-piga mimbara mara moja—Mh.] Atukuzwe Mungu juu Mbinguni! Siwezi kuwazia namna ile ile kamwe, maishani mwangu mwote, nilipoona. Sasa, sijui nini. . . Ninajua hatua hiyo nyingine pale, lakini sijui vile, jinsi ya kufasiri hilo. Haitachukua muda mrefu. Nimeandika hapa, wakati jambo hilo lilipotukia, kama unaweza kuona hapa, “Simama. Usiendelee mbele zaidi ya hili hapa.” Mimi sina sababu ya kuwa mshupavu wa dini. Ninasema tu ile Kweli.

262 Lakini mnakumbuka kile kiatu kidogo, ambapo kila mara nimejaribu kueleza jinsi ambavyo nafsi ilivyokuwa karibu na kitu *kitu fulani* na dhamira ya ndani, na mambo yote ya namna hiyo? Jambo ambalo, lilisababisha tu kundi kubwa la waigaji nyuma yake. Jinsi ambavyo inawabidi kuchukua mkono, na kuwashika watu, na kuwa na mtetemeko? Kila mtu alikuwa na mtetemeko mikononi mwao.

263 Lakini mnakumbuka, wakati Yeye aliponipandisha kule, na kusema, “Huu ndio ule Mvuto wa Tatu, wala hakuna mtu atakayeujua Huo.” Mnakumbuka jambo Hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Maono hayakosei kamwe. Hayo ni kweli kabisa.

264 Sasa angalieni. Mnakumbuka lile ono la lile kundi? Charlie, mimi. . . Hili hapa.

265 Jambo fulani linaendelea, niliwaambia, juma hili, ya kwamba wewe. . . Limekuwa karibu yenu kila upande, lakini sijui kama mliliona.

266 Mnakumbuka lile kundi, la lile ono la Malaika, nilipoondoka hapa kwenda Arizona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnakumbuka “*Ni Saa Ngapi, Mabwana?* [“Amina.”—Mh.] Mnalikumbuka hilo? Angalia, kulikuwa na mlipuko mmoja mkubwa wa ngurumo, na Malaika saba wakatokea. Hilo ni kweli? [“Amina.”] Mlipuko mmoja wa ngurumo, Malaika saba wakatokea.

*Kisha nikaona hapo Mwana-Kondoo wakati alipofungua muhuri wa kwanza, nikasikia mmoja wa*

*wale wenye uhai wanne akisema, kama kwa sauti ya ngurumo, Njoo uone.*

267 Angalia, ngurumo moja, Jumbe Saba ambazo zimekuwa zimetiwa muhuri na haziwezi kufunuliwa mpaka siku ya mwisho, ya wakati huu. Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

268 Sasa, mmeona sehemu ya ajabu ya juma hili? Ndio Hilo. Imekuwa ndio Hilo. Haikuwa ni mwanadamu, m—mtu. Imekuwa ni wale Malaika wa Bwana. Angalia.

269 Kuna mashahidi, watatu, wameketi hapa, ambao juma moja lililopita, kidogo zaidi ya juma moja lililopita, nilikuwa kule juu, huko nyuma kabisa milimani, karibu na Mexico, pamoja na ndugu wawili wanaoketi hapa. Nilipokuwa nikitoa magugu, ama makwekwe, kutoka kwenye mguu wangu wa suruali ndefu; ndipo mlipuko ukatokea, ambao karibu, ilionekana kama, uliitikisa milima nusura uanguke. Sasa, hiyo ni kweli. Sikuwaambia ndugu zangu hata, bali waliona tofauti.

270 Naye akaniambia, “Sasa kuwa tayari. Nenda maawio ya jua. Hii hapa tafsiri ya lile ono.” Unaona? Sasa, ili kuwajulisha, Ndugu Sothmann hakupata yule mnyama aliyekuwa anamtafuta. Tulikuwa tukijaribu kumtafutia. Naye akasema, “Sasa, usiku wa leo, kama ishara kwako, yeye hatampata. Hamna budi kujiweka wakfu wakati huu kwa ajili ya kuzuru kwa Malaika hawa.” Nami nikajisikia nimetoka kwenye fahamu zangu, mnakumbuka.

271 Nami nilikuwa magharibi. Hao Malaika walikuwa wakija mashariki. Nao walipokuja hapo, nilitwaliwa pamoja Nao, (mnakumbuka jambo hilo?) nikija mashariki. [Kusanyiko lilisema, “Amina.”—Mh.]

272 Na Ndugu Fred, aliye hapa usiku wa leo, ni shahidi, na Ndugu Norman. Tulipokuwa tukishuka, karibu nimshawishi mtu huyo abaki na ampate mnyama wake. Hiyo ni kweli, Ndugu Sothmann? [Ndugu Fred Sothmann, “Amina.”—Mh.] Ndiyo, huyo, amesimama yule pale. Nilimshawishi; lakini, hata hivyo, Yeye akasema, “Hatampata.” Sikusema kitu; nikaenda zangu.

273 Jambo fulani, nikiketi kando ya hema, ile siku ambapo. . . Mnakumbuka, Ndugu Sothmann. Nami, mara baada ya kuambiwa mambo fulani, kwamba nilikuweka wewe pamoja na Ndugu Norman. . . Yuko wapi Ndugu Norman? Kule nyuma. Nikawaapisha, ya kwamba hawatasema jambo lililokuwa linatukia. Hiyo ni kweli? [Hao ndugu wanasema, “Amina. Hiyo ni kweli.”—Mh.] Je! niligeuka na kuondoka kwenye hiyo hema namna *hiyo*? Hiyo ni kweli? [“Hiyo ni kweli.”]

274 Kwa sababu, hivi ndivyo ilivyokuwa, barabara kabisa vile ilivyokuwa hasa, na nikijua ya kwamba nisingeweza kulisema mpaka litakapotendeka, nione kama watu wangefahamu jambo hilo.

275 Na je! mliona? “Yule Malaika mmoja,” nilisema, “pale ndani, alikuwa ni Malaika wa ajabu.” Alimaanisha kitu cha zaidi kwangu kuliko Hao wengine wote. Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko, “Amina.”] Walikuwa katika kundi; watatu upande mmoja, na mmoja upande wa juu. Na yule aliyekuwa karibu nami sana hapa, nikihesabu kutoka kushoto kwenda kulia, angekuwa ndiye Malaika wa saba. Yeye alikuwa anang’aa zaidi, alimaanisha kitu cha zaidi kwangu kuliko hao Wengine wote. Mnakumbuka? Nikasema, “Alikuwa ametokeza kifua chake mbele, namna *hiyo*, naye alikuwa anaruka kuelekea mashariki” (mnakumbuka) “namna *hiyo*.” Nilisema, “Walinichukua; wakaniinua juu.” Mnakumbuka jambo hilo? [“Amina.”]

276 Huyu hapa, ndiye mwenye Muhuri wa Saba, jambo ambalo limenishangaza maishani mwangu mwote. Amina! Hiyo mihuri mingine ilimaanisha mengi kwangu, bila shaka, lakini, loo! hamjui kile Huu umemaanisha, kwa mara ya kwanza maishani mwangu! [Ndugu Branham alipigapiga mbimbarani mara kadha wa kadha—Mh.]

277 Niliomba, nikamlilia Mungu. Ni—ni—ni...Baada ya mkutano ule wa Phoenix...Ye yote wa hao watu, pale pamoja nami, anajua. Nililala milimani.

278 Asubuhi moja, niliamka nikapanda kwenda juu kwenye Magenge Marefu ya Sabino, ile milima mikubwa, mirefu yenye magengemagenge. Nami nikapanda kule juu. Na kuna kinjia kidogo cha miguu, ukiisha kuiacha njia, ikipanda juu kwenda Mlima Lemmon, ambao ni mwendo wa miguu wa maili thelathini, karibu futi thelathini za theluji kule juu. Kwa hiyo, kule juu mlimani, asubuhi na mapema kabla ya mapambazuko, nikipanda juu kupitia kwenye kijinjia hiki kidogo cha miguu, chenye miamba iliyotandaa. Nilijisikia nikiongozwa kugeuka upande *huu*. Nami nikageuka, na nikapanda juu kwenye miamba mikubwa iliyochongoka, loo, jamani! yenye urefu wa futi mia kadha.

279 Nami nikapiga magoti katikati ya miamba ile. Nikaweka chini Biblia *hii*, kisha nikaweka kitabu hiki chini...kibao *hiki* kidogo. [Ndugu Branham anaonyesha Biblia yake na kile kibao—Mh.] Nikasema, “Bwana Mungu, ono hili lina maana gani? Mimi—mimi—mimi...” Nikasema, “Bwana, ni... Je! linamaanisha kifo changu?”

280 Mnakumbuka, niliwaambia, “Nilidhani huenda ilimaanisha kifo changu, maana kitu fulani kilipasuka kwa kishindo hata kiliniogopesha nusura nizimie kwa hofu.” Mnakumbuka jambo hilo. Ni wangapi wanaojua jambo hilo, wamelisikia? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mbona, hakika, unaona, ninyi nyote. Nami nilifikiri lingeweza kumaanisha mauti yangu.

281 Na halafu katika kile chumba, nilisema, “Ilikuwa... I—i—ilikuwa ni kitu gani, Bwana. Ina—ina maana gani? Je!

inamaanisha nitakufa? Kama ndivyo, sawa, sitaiambia familia yangu. Hebu niondoke tu, unaona, kama kazi yangu imekwisha.” Ndipo nikasema . . .

<sup>282</sup> Sasa, ilikuwa ni kitu gani? Lakini Yeye alirudisha ushuhuda, mnakumbuka nikiwaambia, ya kwamba haikuwa ni jambo hilo. Ilikuwa ni kuendelezwa kwa kazi yangu. Loo! loo! loo! Mnalipata? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Unaona? Na nikiketi juu huko katika Magenge Marefu ya Sabino . . .

<sup>283</sup> Baba wa Mbinguni anajua jambo hili. Hakika tu kama vile mmeona jambo hilo likitimia, Malaika wale walishuka moja kwa moja na kuthibitisha kila Ujumbe kwamba ni sawa. Basi, mnajua kama unatoka kwa Mungu, ama hapana. Ulitabiriwa, kwenu, kwa ono. Nisingeweza kuwaambieni mpaka mwisho wa ibada hizi, maana nilikatazwa kuwaambia.

<sup>284</sup> Katika Magenge Marefu ya Sabino, nikiwa nimeketi kule asubuhi hiyo, nilikuwa nimeinua mikono yangu. Na ninii yangu . . . Upepo ulikuwa umeiangusha kofia yangu nyeusi kuukuu ya kale chini. Wakati . . . Nilipokuwa nimesimama pale, huku nimeinua mikono yangu, nikiomba. Nikasema, “Bwana Mungu, hili lina maana gani? Siwezi kulielewa, Bwana. Nifanye nini? Kama ndio wakati wangu wa kwenda Nyumbani, jalia nipande hapa juu, ndipo mahali wao hawataweza kuniona. Sitaki mtu ye yote awe anaomboleza, kama ninaondoka. Na—nataka jamaa yangu ifikiri ya kwamba niliondoka nikaenda tu kutembea. Nao hawataniona. Nifiche mahali fulani. Kama itanibidi kuondoka, mbona, jalia niondoke. Labda Joseph ataikuta Biblia yangu imekaa hapa, siku moja, na umjalie aitumie. Unaona, kama ninaondoka, jalia niondoke, Bwana.” Nami nilikuwa nimenyosha mikono yangu. Na, mara, kitu fulani kikagusa mkono wangu.

<sup>285</sup> Sijui. Siwezi kusema. Nililala usingizi? Sijui. Nilingia katika njozi? Sijui. Je! ilikuwa ni ono? Siwezi kuwaambia. Jambo pekee ninaloweza kusema ni vile mimi . . . Ni kitu kile kile kama hao Malaika walivyokuwa!

<sup>286</sup> Nao ukaangukia mkononi mwangu. Nami nikaangalia, nao ulikuwa ni upanga. Nao ulikuwa na mpini wa lulu, mzuri sana; na ulikuwa na kinga juu yake, ya dhahabu. Na ubaba wake ulionekana kitu kama kromi, kama fedha, ila tu ulikuwa unang’aa sana. Nao ukali wake ulikuwa kama ncha ya unyoya, loo, jamani! Basi nikawazia, “Je! hicho si ndicho kitu kizuri kuliko vyote!” Unaenea tu mkono wangu barabara! Nikawaza, “Huo ni mzuri sana. Lakini,” nikasema, “jamani, kwa kawaida mimi ninaogopa vitu hivyo, upanga.” Nikawaza, “Nitafanya nini na huo?”

<sup>287</sup> Na mara Sauti ikashuka kupitia mahali pale na kupatikisa, ambayo ilitikisa miamba. Kasema, “Ni ule Upanga wa yule Mfalme!” Ndipo nikatoka kwenye ono hilo.

288 “Ule Upanga wa yule Mfalme.” Sasa, kama Hiyo ingesema, “Upanga wa mfalme. . .” Lakini ilisema, “Ule Upanga wa yule Mfalme.” Na kuna mmoja tu aliye “yule Mfalme,” na huyo ni Mungu. Naye ana Upanga mmoja, huo ni Neno Lake, ambalo nimeishi kwalo. Kwa hiyo, ninasema kweli, Mungu; nikiwa nimesimama kwenye dawati Lake takatifu hapa, nikiwa na Neno hili takatifu limewekwa hapa! Ni Neno! Amina! Loo, ni siku ya namna gani tunayoishi! Ni jambo kuu jinsi gani! Mnaona lile fumbo na siri? Ule wa Tatu. . .

289 Nikisimama pale wakati hili liliponiacha, Kitu fulani kilinjia tu na kusema, “Usiogope.” Sasa, sikusikia sauti yo yote. Ni kama ilinena kutoka ndani yangu. Sina budi nanibidi tu kuwaambia kweli, vile vile hasa ilivyotukia. Kitu fulani kilinigusa, na kikasema, “Usiogope. Huu ndio ule Mvuto wa Tatu.”

290 Mvuto wa Tatu! Mnaukumbuka? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Alisema, “Umekuwa na waigizaji wengi sana kwenye jambo hili, yale uliyojaribu kuelezea. Lakini,” kasema, “hata usijaribu, Huu.” Mnaukumbuka hilo? Ni wangapi wanaukumbuka lile ono? [“Amina.”] Mbona, liko kila mahali. Limerekodiwa, na kila mahali. Hiyo ilikuwa kama miaka sita iliyopita, miaka saba iliyopita. Ilikuwa miaka saba iliyopita. Kasema, “Usijaribu kuelezea jambo Hilo.” Kasema, “Huu ndio ule Mvuto wa Tatu, lakini nitakutana nawe kule ndani.” Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Akasema, “Usijaribu. . .”

291 Nilikuwa nimesimama na ki—kijiatu cha mtoto mchanga, wakati Yeye aliponiambia. Kasema, “Sasa fanya Mvuto wako wa Kwanza. Na utakapofanya hivyo, samaki watakimbia chombo.” Kasema, “Halafu angalia Mvuto wako wa Pili,” kasema, “kwa maana Huo utakuwa tu ni samaki wadogo.” Akasema, “Ndipo ule Mvuto wa Tatu utampata.”

292 Na hao wahudumu wote wakanizunguka, wakasema, “Ndugu Branham, tunajua unaweza kufanya jambo hilo! Haleluya! Ndugu Branham!” Hapo ndipo daima mimi hufungwa, na kundi la wahubiri. Unaona? Napenda watu. Wao wanakutaka ueleze kila kitu, *hiki, kile*.

293 Nami nikasema, “Vema, eh, eh, eh,” nikasema, “sijui.” Nikasema, “Ninajua kuvua samaki. Sasa,” nikasema, “sasa, jambo la kwanza unalofanya. . . Hivi ndivyo inavyofanyika. Unaona samaki wote pande zote; huna budi kushtua chombo ghafla.” Vema, hizo ndizo mbinu hasa za kuvua samaki. Kwa hiyo nikasema, “Shtua chombo. Sasa, unaona, niliposhtua chombo, mara ya kwanza, sasa samaki wanaifuata.” Lakini walikuwa ni wadogo. Na hao ni kama tu wale wao waliokuwa wakiwashika.

294 Kwa hiyo basi ni—nikasema, “Ndipo mta—mtaweka. . .” Basi nikaishtua kuitoa ghafla, ukingoni. Nami nilimpata samaki,

lakini alionekana kama ngozi juu ya chambo, alikuwa tu... alikuwa ni mdogo sana.

<sup>295</sup> Halafu nilikuwa nimesimama pale, na Kitu Fulani kikasema, “Nilikuambia usifanye hivyo!”

<sup>296</sup> Nikaanza kulia. Kamba yote ya ndoano ilikuwa imenizongazonga, namna *hii*. Nami nilikuwa...nilikuwa nimesimama pale, nikilia, huku nimeinamisha kichwa changu chini namna *hiyo*. Nikasema, “Mungu! Loo! mimi... Nisamehe! Mimi—mimi ni mtu mjinga. Bwana, usininii... Nisamehe.” Nami ni—nilikuwa na kamba hii.

<sup>297</sup> Na hicho, nilichokuwa nimeshika mkononi mwangu, kilikuwa ni kiatu kidogo cha mtoto mchanga, kirefu kama *hivi*. Nami nilikuwa na kamba hiyo, yenye karibu unene wa kidole changu, kama nusu inchi, karibia hivyo. Na kile kitundu katika kiatu hiki kilikuwa na ukubwa wa...kidogo kuliko mo—moja ya kumi na sita, labda, ya inchi, kwenye kile kijitundu. Nami nilikuwa nikijaribu kukifunga kijiatu hiki kwa kamba hii kubwa mno yenye unene wa inchi moja. Loo!

<sup>298</sup> Sauti ikaja, ikasema, “Huwezi kuwafundisha watoto wachanga wa Kipentekoste mambo ya kimbinguni.” Kasema, “Sasa, achana nao!”

<sup>299</sup> Na mara tu Yeye akanipandisha juu. Akanipandisha juu, na kuniketisha huko juu sana, mahali ambapo mkutano ulikuwa unaendelea. Ilionekana kama hema ama kanisa kubwa la jimbo, la namna fulani. Nami nikaangalia, na kulikuwa na kijisanduku, kitu kama hicho, mahali padogo upande mmoja. Nami nikaona hiyo Nuru ilikuwa ikinena na mtu fulani, aliyekuwa juu yangu, ile Nuru mnayona pale kwenye ile picha. Ilizunguka ikaondoka kwangu, namna *hiyo*, na ikaenda juu ya ile hema. Kisha akasema, “Nitakutana nawe kule.” Halafu akasema, “Huu utakuwa ni ule Mvuto wa Tatu, nawe hutamwambia mtu ye yote.”

Na kwenye Magenge Marefu ya Sabino, Yeye alisema, “Huu ndio ule Mvuto wa Tatu.”

<sup>300</sup> Na kuna mambo matatu makubwa yanayoambatana Nao. Na moja lilifunuka leo...ama jana; lile lingine limefunuka leo; na kuna jambo moja ambalo siwezi kufasiri, kwa maana liko katika lugha isiyojulikana. Lakini nalisimama pale pale na kuliangalia moja kwa moja. Na huu ndio ule Mvuto wa Tatu unaokuja. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara tatu—Mh.] Na Roho Mtakatifu wa Mungu... Loo, jamani!

Hiyo ndiyo sababu Mbingu nzima ilinyamaza.

<sup>301</sup> Sasa, a—afadhali niachie papa hapa, unaona. Na ninii tu—najisikia tu nikisimamishwa, nisiseme zaidi juu Yake. Mnaona?

<sup>302</sup> Kwa hiyo, kumbukeni tu, ule Muhuri wa Saba, sababu ya kutokufunguliwa. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani



mara sita—Mh.] Unaona, sababu ya Huo kutofunuliwa, hakuna mtu anayepaswa kujua habari Zake.

303 Nami nawatakeni mjue, kabla hata sijapata kujua Neno lo lote juu ya Huo, ono hilo lilikuja miaka mingi iliyopita. Mnakumbuka jambo hlo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na ndio Huu hapa, kama tu hii mingine ilivyofanya, unaingia moja kwa moja kwenye Neno pale pale hasa ulipokuwa. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara mbili.] Na Mungu anajua moyo wangu, sijawaza jambo kama Hilo hata mara moja, na likawa ndio Hili. Muda umeendelea kuliko tunavyodhania. A-ha. Loo, jamani!

304 Hiyo inaonyesha Hilo linatoka kwa Mungu, kwa kuwa, unaona, linalingana kabisa katika ahadi za Mungu, kutoka kwenye ule mwisho wa U—Ujumbe. Unaona. Angalia sasa, kwa ajili ya Ujumbe wa wakati wa mwisho, Muhuri huu. Hata hivyo, Yeye—Yeye ameifunua Mihuri yote sita, lakini Yeye hasemi Neno juu ya ule wa Saba. Na ule Muhuri wa wakati wa mwisho, hapo utakapoanza, utakuwa ni siri kabisa, kulingana na Biblia, kabla ya kujua jambo Hilo. Na kumbukeni, Ufunuo 10:1-7, 1 hadi 7, Mlango wa 10:1 hadi 7, “Mwishoni mwa Ujumbe wa malaika wa saba, siri zote za Mungu zitajulikana.” Tuko katika wakati wa mwisho, kule kufunguliwa kwa Muhuri wa Saba.

305 Sasa, nilijua? Juzijuzi, Jumapili iliyopita, juma moja limekwisha leo, wakati nilipokuwa nikihubiri juu ya “Iweni wanyenyekevu! Iweni wanyenyekevu! Kumbukeni, Mungu hutenda kazi katika mambo madogo.” Sikutambua kile ulichokuwa ukizungumzia hasa. Na sasa ninaliona. Liko katika njia nyenyekevu sana! Ungefikiria ya kwamba jambo kama hilo lingefunuliwa Vatican ama. . . Lakini linakuja kama tu Yohana Mbatizaji. Linakuja kama kuzalizwa kwa Bwana wetu, katika hori. Utukufu kwa Mungu! Nasema kweli, ile saa imekaribia! Amina! Tuko hapa. Loo, jamani!

306 Sasa je! mnaona jambo hilo, Kweli ya ono la Mungu, wale Malaika saba wakinileta kutoka magharibi? Wao walikuwa wakitoka macheo ya jua, wakirudi maawio ya jua, wakinileta hapa kwa ajili ya Ujumbe huu usiku wa leo. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara mbili—Mh.] Loo, jamani!

307 Sasa, Sauti ya hiyo ngurumo kubwa, na utume ulioletwa hapa, imefunuliwa, ya kwamba Huo. . . na kuthibitisha ya kwamba ilikuwa ni Mungu. Wazieni tu sasa. Mimi sikujua Mihuri hii, nayo imefunuliwa juma hili. Je! kuna mtu aliyewazia jambo hilo, la hao Malaika saba kuwa ndio Huu, kwamba ndio Ujumbe ambao ulikuwa unakuja, hao malaika wakinirudisha hapa kwa ajili ya Huo? Unaona?

308 Kumbukeni, yule Mjumbe wa saba alikuwa. . . Wale Wajumbe sita walikuwa. . . Yule mashuhuri sana kwangu, yule Malaika wa saba, alionekana na cha zaidi kwangu kuliko ye

yote yule. Sasa, unaona, wao walikuwa wamesimama namna *hii*. Sasa, tunataka tu mwangalie. Nami nilikuwa nimesimama *hapa*, nami nilikuwa nikiwaangalia wale wengine. . .

<sup>309</sup> Unaona, mmoja, lile kundi la kwanza, la ndege wadogo, mabawa yamechoka sana. Mnawakumbuka? Nao wote waliruka kwenda mashariki. Na lile kundi la pili, walikuwa ndege wanaong'aa zaidi, wakubwa zaidi, walionekana kama hua, wenye mabawa yaliyochongoka. Waliruka kuelekea mashariki. Mvuto wa Kwanza, Mvuto wa Pili, halafu lililofuata walikuwa ni Malaika. Na wakati. . .

<sup>310</sup> Nilikuwa nimesimama pale pale, na mlipuko huu ukaondoka. Nami nilikuwa nimeangalia upande *huu*, kuelekea magharibi, Nao wakaja na kunitwaa tu, ndani pale. Ndipo nikatoka kwenye fahamu zangu kabisa. Na mmoja Wao, akija, ndiye aliyeonekana wa ajabu sana kwangu, ndiye aliyekuwa kwenye mkono wangu. . . Alikuwa upande wa kushoto, mahali nilipoingilia kwenye lile kundi. Lakini nikihesabu kutoka kushoto kwenda kulia, angekuwa ndiye yule Malaika wa saba, unaona, akija kutoka upande mmoja kwenda mwingine. Sasa, kumbukeni, wale Wajumbe saba.

<sup>311</sup> Je! mnakumbuka ile piramidi ya Mwamba mweupe, wa ndoto ya Junior Jackson ambayo niliwafasiria? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona? Angalia, usiku ule nilioondoka, na ni-. . . Kulikuwa na ndoto sita zilizokuja, na kila moja ya hizo inazungumzia jambo lile lile. Ndipo lile ono likaanza, na likanituma magharibi. Na, Junior, yeye alikuwa akiangalia wakati. . . Angalia. Angalia jinsi lilivyo kamilifu!

<sup>312</sup> Sasa, nina—ninatumaini na kuamini ya kwamba ninyi watu mnatambua ya kwamba ninajaribu kuweka neema hii juu ya Yesu Kristo, Ambaye ndiye Mwazilishi wa yote Hayo. Na sababu pekee ambayo hamjanisikia nikizungumza namna hii hapo nyuma, maishani mwenu, lakini saa hii inakaribia. Unaona? Angalieni.

<sup>313</sup> Sasa kulihakikisha, kwenu, ili kwamba liweze kuzama ndani. Ninajitayarisha kuwaacha tena. Sijui nitaenda wapi. Sina budi kuhubiri Injili mahali pengine. Lakini sasa, ile. . .

<sup>314</sup> Huenda mkasema, "Nimesikia aina yote hiyo ya ushupavu wa dini." Sijui nini; siwezi kumhukumu mtu mwingine ye yote.

<sup>315</sup> Inanibidi tu kuwajibika kwa Mungu kwa yale mimi. . . kwa—kwa ajili yangu. Lakini kulikuwapo na wakati mmoja wo wote niliowahi kuwaambia jambo lo lote katika Jina la Bwana, ambalo halikuwa sahihi, katika miaka hii yote? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Hakuna mtu mwingine ye yote anayeweza kusema hivyo, kwa sababu daima nililisea jinsi tu Yeye alivyolisema.

<sup>316</sup> Sasa hebu niwaonyeshe tu ya kwamba hii ni kweli kabisa, na kulithibitisha.

317 Sasa kumbukeni, “Kama kuna wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitasema naye katika maono, na kumjulisha kwa ndoto.” Kufasiri ndoto, ndiko huko. Yusufu, yeye aliweza kufasiri ndoto, na kunena na—na kuona maono. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

318 Sasa angalia jambo hili. Kwamba, sasa, wakati jambo hili lilipotukia, Junior alikuwa amesimama kwenye uwanja fulani ambao ulikuwa—ulikuwa na piramidi kubwa ndani yake, namna hiyo. Na kulikuwa na jambo fulani lililokuwa limeandikwa kwenye miamba, nami nilikuwa nikiwafunulia watu jambo Hilo. Hiyo ni kweli, Junior? [Ndugu Junior Jackson anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Yapata mwaka mmoja kabla halijatukia.

319 Basi angalia jambo linalofuata sasa. Nilichukua namna fulani ya mtaimbo na nikaikata na kuiondoa, na hapo ndani palikuwapo na Mwamba mweupe ambao haukuandikwa kitu cho chote juu Yake. Na, kwenye wakati huo, nikaondoka kuelekea magharibi. Nami nilikawaambia hao wote, nilisema, “Msiende magharibi. Kaeni hapa na mwuangalie Huu mpaka nitakaporudi.” Nikaenda magharibi, kwa ajili ya ule mlipuko; nikarudi mashariki, na Roho Mtakatifu akifasiri Neno hili lisiloandikwa. Sasa, kama huyo si Mwenyezi Mungu kikamilifu, ninataka mjue ni nini.

320 Kwa sababu gani ninasema jambo hili, marafiki? Ni kuwaonyesha tuko kwenye wakati wa mwisho. Sasa, kama hiyo mingine iko barabara kwenye Neno, vivyo hivyo na Huu uko barabara kwenye Neno! Tumewasili. Tuko mwisho, marafiki.

321 Bado kidogo itakuwa “wakati umekwisha.” Mamilioni watapoteza maisha yao. Mamilioni watayapoteza, ambao sasa wanaamini ya kwamba wameokolewa, watahesabiwa kama chakula cha wakati wa atomiki. Tunaishi katika saa ya mwisho. Kwa neema ya Mwenyezi Mungu, kwa msaada Wake kwa watu Wake, ili kwamba wakutarajie kule kuonekana upesi kwa Kristo! “Ni muda gani, Ndugu Branham?” Labda miaka ishirini; labda katika miaka hamsini; labda katika miaka mia moja. Sijui. Na labda asubuhi; labda tena usiku wa leo. Sijui. Na mtu ye yote akisema wanajua, wanakosea. Unaona? Hawajui. Mungu, peke yake, anajua.

322 Sasa angalia. Nasema kweli, Mungu, ninasema Kweli, ya kwamba Haya yamepambanuliwa kiroho kwangu mimi, yamepambanuliwa na Roho Mtakatifu. Na, kwa kila moja ya Hayo, limejitambulisha mahali Pake katika Biblia.

323 Sasa, kwamba hii siri kubwa ambayo iko chini ya Muhuri huu ni nini, Sijui. Sijui. Nisingeweza kuifahamu. Nisingeweza kuitambua Hiyo, yale—yale tu iliyosema, lakini najua ya kwamba ilikuwa ni hizo Ngurumo Saba zikifuatana mfululizo kutoa sauti zao moja baada ya nyingine, zikinguruma tu mara saba mbalimbali. Nazo zilifunua jambo lingine nililoona.

Halafu, nilipoona jambo Hilo, nilitafuta fasiri yake. Ilipita pale, nami sikuelewa ni kitu gani. Hiyo ni kweli kabisa. Unaona? Saa Yake ingali bado haijafika.

324 Lakini, inasogea kwenye duara ile, unaona. Inakaribia. Kwa hiyo, jambo mnalopaswa kufanya ni kukumbuka ya kwamba ninasema nanyi katika Jina la Bwana. Iweni tayari, kwa kuwa hamjui ni wakati gani jambo fulani linaweza kutukia.

325 Sasa, jambo hilo litakapoingia kwenye kanda, ambalo linaingia, hilo labda litawafanya maelfu ya rafiki zangu kuniacha. Maana, wao watasema, ya kwamba, “Ndugu Branham anajaribu kujiweka, na kujifanya, m—mtumishi ama nabii, ama kitu fulani, mbele za Mungu.” Hebu niwaambieni, ndugu zangu, hilo ni kosa.

326 Ninawaambia tu jambo nililoona na yale niliyoambiwa. Na sasa wewe—wewe fanya lo lote unalotaka kufanya. Sijui ni nani atakayeninii. . . yale yatakayotukia. Sijui. Ninajua tu ya kwamba hizo Ngurumo Saba zinashikilia ile siri. Mbingu Zilikuwa kimya. Kila mtu anaelewa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Huenda ikawa ni wakati umefika, huenda ikawa wakati umewadia sasa, ambapo mtu huyu mkuu ambaye tunamtarajia ajitokeze jukwaani anaweza atokee jukwaani.

327 Labda huduma hii, ambayo nimejaribu kuwarudisha watu kwenye Neno, imeweka msingi; na kama imeweka, nitawaacha, kabisa. Hatutakuwa sote wawili hapa kwa wakati mmoja. Mnaona? Kama ndivyo ilivyo, yeye atazidi, nami nitapungua. Sijui.

328 Lakini nimetunukiwa, na Mungu, kuangalia na kuona ilikuwa ni kitu gani, unaona, kuona ikifunuliwa kufikia kiasi hicho. Sasa, hiyo ni Kweli.

329 Nami nina hakika mmeona mambo ambayo yamekuwa yakitendeka juma hili. Nina hakika mlimwona maskini mvulana huyo mdogo wa Collins aliyelala pale, akifa, juzi usiku; maskini yule msichana mdogo mwenye lukemia.

330 Ufalme wa Mungu unakuja. Nao unakuja zaidi na zaidi kutoka kwenye kivuli kuingia kwenye kitu uhalisi, kama vile ulivyokuwa. Sasa, hilo halipaswi kuwakaba watu roho. Kutoka kuhesabiwa haki, kutakaswa, hadi kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, na halafu *hapa, hapa*. Mnaona? Tunamkaribia tu Mungu zaidi, wakati wote.

331 Je! hamwezi kuona, enyi wahudumu wa Kimethodisti, jinsi ambavyo ujumbe wenu wa utakaso ulivyokuwa ni wa juu zaidi ya ule aliohubiri Luther?

332 Enyi Wapentekoste, hamwezi kuona ujumbe wenu wa ubatizo uko juu zaidi ya ule Wamethodisti waliohubiri? Mnajua ninalomaanisha?

333 Loo! tumekuwa na mambo mengi sana yaliyotukia! Na hiyo ni kweli. Na kama kuna mtu ye yote anayechukia mabaya, na watu kusema jambo ambalo kweli ni uongo wala si Kweli, ninachukia jambo hilo.

334 Lakini mimi—mimi napenda Kweli iliyo halisi, haidhuru inaingilia *hivi* ama *vile* kiasi gani. Kama ni Kweli, Mungu hatimaye ataionyesha kwamba ni Kweli. Na kama Yeye hatendi jambo hilo, moja ya siku hizi hivi karibuni, basi ono langu halikuwa la kweli. Sasa mnaona mahali ambapo nilijiweka mimi mwenyewe.

335 “Itakuwa lini, Ndugu Branham?” Siwezi kuwaambia. Sijui.

336 Lakini, moja ya siku hizi, kama tusipokutana kamwe tena katika dunia hii, tutakutana kule ng’ambo kwenye kile—kwenye kile kiti cha hukumu cha Kristo. Nanyi mtaona, ya kwamba, katika chumba kile, ule ufunuo uliokuwa ukitoka kwa Mungu, kama vile tu huo mwingine ulivyotoka, ya kwamba Hiyo... Moja ya zile siri za Muhuri ule, sababu ya kutofunuliwa Kwake, ilikuwa ni Ngurumo Saba zilizotoa sauti Zao. Na ndio huo hapo, barabara. Kwa sababu, hakuna kitu kinachojua lo lote juu Yake. Hata haukuandikwa. Kwa hiyo, tuko katika wakati wa mwisho. Tumewasili. Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya Neno Lake.

337 Ninamshukuru Yeye kwa ajili ya Yesu Kristo. Kwa maana, bila ya Yeye kumtuma kwa ajili ya—ya upatanisho wa dhambi zetu, sote tungekuwa katika kinyaa kikubwa cha dhambi, bila tumaini. Lakini, kwa neema Yake, Damu Yake—Yake husafisha dhambi yote. Ni kama tu tone la wino katika ndoo ya Kloroksi, hungeweza kuuona huo wino tena. Wakati dhambi zetu zinapotubiwa, zinawekwa katika Damu Ya Yesu Kristo; hazitajulikana tena. Mungu huzisahau; hata hazijatendwa kamwe. Na mradi tu hiyo dhabihu iko pale katika upatanisho kwa ajili yetu, basi yatosha. Imekwisha, unaona. Si—sisi si wenye dhambi tena. Sisi ni Wakristo, kwa neema ya Mungu. Kumbukeni, sisi wenyewe kama tulivyo labda tungekuwa wabaya tu kama tulivyowahi kuwa. Lakini, unaona, neema ya Mungu imetokea kwetu, na hiyo ndiyo iliyotufanya vile tulivyo leo, ndugu na dada Wakristo.

338 Hili limekuwa ni juma kuu sana kwangu. Nimechoka. Akili zangu zimechoka. Kwa sababu ni—nimeninii...vizuri nilivyoweza kufanya. Na jambo la ajabu linaendelea, kila siku. Ningeshangaa; kuingia katika kile chumba, na kuwa mle kwa dakika chache, na kuona Kitu fulani kikinigeuza kabisa.

339 Na, hapa, ningeingia kule na kuchukua mihtasari. Ningechukua vitabu vya Dk. Smith, Uriah Smith, na, loo! ninii wote—waandishi na kadhalika, na kusoma humo, kusoma katika vitabu vyao. Ninasema, “Sasa huu *hapa* Muhuri wa Sita. Huu *hapa* Muhuri wa Nne. Sasa mtu huyu anasema nini? Yeye angesema, ‘Vema, ulikuwa ni *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*.’”

Ningeangalia upande huu na kumchukua mtu mwingine. Alisema ilikuwa *kadha na kadha*. Na ilionekana tu kana kwamba mimi nilininii. . . Ilikuwa sivyo. Unaona?

<sup>340</sup> Kisha nikawaza, “Vema, ni nini, Bwana?” Nami ningetembea huku na huku sakafuni kwa muda kidogo. Ningeepiga magoti na kuomba. Ningerudi na kuichukua Biblia; ninaketi chini, ninasoma. Ninatembea huku na huku.

<sup>341</sup> Halafu, mara, nilipotulia, huu hapa ukifunuliwa namna hiyo. Ndipo ningenyakua kalamu upesi sana, na kuanza kuuandika namna hiyo, cho chote nilichokuwa nikiona na kufanya. Nikiuangalia, namna hiyo, mpaka nikamaliza kuandika.

<sup>342</sup> Ndipo ningechukua, siku nzima iliyosalia, na kurudi nyuma na kufuatilia jambo Hili, na kuona kama liliambatana kila mahali huko nyuma katika Maandiko. Halafu. “Thibitisha mambo yote.” Unaona? Nina jambo Hili hapa.

<sup>343</sup> Baadaye nafikiri, “Sasa, kuna watu wengi waliokuwa na maono. Kuna wengi waliopata ufunuo.” Kama ni kinyume cha Neno, liache; hiyo ni kweli, liache.

<sup>344</sup> Sasa, sasa, ndipo ningefuatilia jambo hili hata huko nyuma namna *hii*, kulifuatilia namna *hii*. Ningeandika mambo madogo madogo hapa. Nikawaza, “Vema, sasa, darasa litafurahia kusikia jambo hili, maana linaunganisha *hapa* na kuunganisha *hapa*. Sasa, hebu tuone, hili linasema nini *hapa*? Naam. Na, naam, hili hapa, papa *hapa*.” Unaona?

<sup>345</sup> Na kulirudisha kupitia kwenye Biblia, na kulifunganisha jambo hilo, juma nzima. Hilo hapo, kwenye kanda. Mmekaribishwa kuzichukua. Nami nimefanya jambo hilo vizuri kabisa nijuavyo, chini ya ushirika wa Kikristo, neema ya Mungu, kwa watu wote, kwa Yesu Kristo. Nimefanya vizuri sana nijuavyo.

<sup>346</sup> Mmekuwa moja ya madarasa mazuri sana. Hakuna mtu angaliweza kuketi kiungwana zaidi ya hivyo. Ninyi nyote mmekuja hapa kwenye saa saba mchana, mpaka saa kumi na moja, mpaka wakati wo wote walipofungua kanisa na kuleta ninii. . . kuwaruhusu watu waingie. Mmesimama kwenye baridi; mmekeki kwenye theluji; mmefanya kila kitu; mkasimama kwenye kuta, mpaka miguu yenu ikauma. Ningeona hao wanaume, wameketi chini; wanawaachia wanawake viti. Na watu mbalimbali wangesimama namna hiyo, wameketi hapa na pale. Nikawaza, “Bwana, ninii yote. . .”

<sup>347</sup> Juma hili limekuwa ni la ajabu. Jambo lote limekuwa la kustaajibisha kwa namna fulani, jinsi, wakati watu wanapokuja, kuwaona wakisimama huko nje, kwenye madirisha, milangoni, huko sehemu za huko nyuma, kila mahali, kusikiliza. Na kuhusu kuwa mnenaji, mimi niko mbali na kuwa mnenaji. Ni—nina akili kiasi hicho, kujua ya kwamba mimi

si mnenaji, kwamba mimi si mnenaji. Lakini kwa nini watu wangeketi na kusikiliza namna hiyo? Kwa nini wafanye jambo hilo? Wao hawaji kumsikiliza mtu kama mimi. Lakini wanakuja kwa sababu kuna Kitu fulani ndani yake, kinachowavutia watu Kwake. Unaona? Kuna Kitu fulani ndani yake, kinachowavutia.

<sup>348</sup> Kama vile mke wangu alivyosimama hapa jukwaani na kuimba, wakati nilipoanza:

Wanakuja kutoka Mashariki na Magharibi,  
Wanakuja kutoka nchi ya mbali,  
Kula pamoja na Mfalme, kula kama wageni  
Wake;  
Jinsi hawa wasafiri walivyobarikiwa!  
Wakiutazama uso Wake mtakatifu  
Unaong'aa kwa Nuru ya Kiungu;  
Washiriki watakatifu wa neema Yake,  
Watang'aa kama johari katika taji Yake.

<sup>349</sup> Naomba ushike hilo moyoni mwako daima, “Kuwa johari katika Taji ya Yesu Kristo.” Paulo aliliambia Kanisa, “Ninyi—ninyi ni lulu, johari za Taji Yake.” Tunataka kuwa lulu za Taji ya Yesu Kristo.

<sup>350</sup> Hatutaki, hatutamweka mwanadamu kamwe ndani yake. Sahauni jambo lo lote kunihusu mimi. Mimi ni ndugu yenu, mwenye dhambi aliyekolewa kwa neema, asiyestahili kuishi. Hiyo ni kweli kabisa. Sisemi jambo hilo ili kuwa mnyenyekevu; hayo ni mambo ya kweli. Hakuna kitu cho chote ndani yangu, hakuna hata kitu kimoja kilicho kizima, hata kidogo.

<sup>351</sup> Lakini neema ya Mungu imeruhusu maskini macho yangu yanayoingia giza ya angalie ng'ambo ya pazia la wakati na kuona mambo hayo huko ng'ambo, baadaye nikarudi.

<sup>352</sup> Nilipokuwa mvulana mdogo, niliwapenda watu. Daima nilitaka mtu fulani anipende na kuzungumza nami. Hakuna mtu angefanya hilo, kwa sababu ya jina la jamaa yangu. Hakuna mtu angezungumza nami.

<sup>353</sup> Lakini wakati nilipojisalimisha kwa Mungu, basi...Watu wetu, ukoo wao, wakiwa ni Waairishi, niliwaza, “Labda... Wote walikuwa ni Wakatoliki, na labda hicho ndicho Kitu halisi.” Nilikwenda *kule*, Na Yeye alikuwa kwingine. Kisha nikaenda kwenye kanisa la Kwanza la Kibatisti, pia Yeye alikuwa kwingine.

Nikasema, “Bwana, hapana budi kuna njia ambayo ni ya kweli.”

Na Kitu fulani kikasema, “Ni Neno.”

Nimeshikilia hilo Neno. Angalia kila ono, kila mahali.

<sup>354</sup> Ile siku niliyoweka lile jiwe la pembeni kule, na kuweka kile kule ndani, niliandika humo yale Yeye aliyonionyesha asubuhi ile katika ono. “Uwe tayari, wakati ukufaa na wakati

usiokufaa, karipia, kwa uvumilivu wote na Mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia makundi-makundi, kama waalimu, kwa kuwa wana maskio ya utafiti; nao watajipusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.” Nami nimeiona miti hiyo miwili, niliyosimama karibu nayo, ikifanya jambo lile lile. Hiyo ni kweli. Nasi tunaiona. Na hiyo ni kweli. Na, sasa, ninyi hamtaninii. . .

<sup>355</sup> Kumbukeni. Hebu niwausie tena. Usimwambie mtu ye yote, “Asante,” hata kidogo. Usiseme, usiwazie hilo, mhudumu fulani ama jambo fulani, mwanadamu fulani; ana jema lo lote. Maana, hakuna. Sijali yeye ni nani. Hakuna jambo zuri kwa mtu ye yote. Hiyo ni kweli.

<sup>356</sup> Kama kuna lundo zima la matarumbeta hapa, na moja ya hayo ilikuwa lipige muziki fulani, ni huyo mtu. . . Matarumbeta hayo hayatoi sauti kabisa. Ni mtu huyo anayeweza kupiga hiyo tarumbeta, ndiye anayejua atakalofanya, ambaye anaichukua hiyo tarumbeta. Hiyo tarumbeta haina uhusiano wo wote na jambo hlo. Sauti inatoka kwenye akili iliyo nyuma yake. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, matarumbeta yote ni sawa.

<sup>357</sup> Watu wote ni sawa. Wakristo wote ni sawa. Hakuna watu wakuu miongoni mwetu. Sisi si watu wakuu, si wanawake wakuu. Sisi sote ni ndugu na dada, wote tu sawa, katika kundi moja. Sisi si “wakuu.” Mmoja hamfanyi mwingine mkubwa zaidi kuliko huyo mwingine, hana uhusiano wo wote, nalo. La, bwana. Lakini sisi sote ni wanadamu tu.

<sup>358</sup> Usijaribu kufafanua mambo. Usijaribu kufanya lo lote zaidi ya kuishi maisha mazuri, ukimpa Yesu Kristo sifa na heshima. Kila mtu anafahamu na jambo hilo sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Amina. Mpende kwa moyo wako wote. Unampenda? [“Amina.”]

Nampenda, (Na nitampenda!), nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>359</sup> Mungu asifiwe! Kila mtu anaelewa kwelikweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kila mtu anaamini? [“Amina.”] Kumbukeni wakati kwanza nilipoanza, “Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Mkono wa Bwana umefunuliwa nani?” Je! Yeye amekufunulia, rehema Yake, wema Wake? [“Amina.”] Amina. Kumbukeni tu, mpendeni kwa moyo wenu wote.

<sup>360</sup> Ninarudi nyumbani sasa. Nitarudi hapa tena, Bwana akipenda, kwenye tarehe moja Juni.

<sup>361</sup> Pengine, kama Bwana akiliweka moyoni mwangu, labda wakati fulani mnamo majira haya ya mwanzoni mwa kiangazi, kama Juni ama wakati wo wote ule, labda mapema mwishoni mwa mwaka, kama Bwana akikawia, ningetaka kurudi na



kuketi siku nyingine saba usiku, kwa ajili ya zile Baragumu Saba za mwisho. Mngetaka jambo hilo? Mngetaka hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mtaniombea, kwamba Mungu atanisaidia? [“Amina.”] Sawa.

<sup>362</sup> Hata nitakapokutana nanyi tena, kumbukeni wimbo huu mzuri wa kale:

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na akanunua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>363</sup> Sasa nawataka mwinamishe vichwa vyenu. Ninataka kuwaombea. Kabla mchungaji hajawaruhusu kuondoka, ninataka kuwaombea.

<sup>364</sup> Baba yetu wa Mbinguni, wajalie watu hawa, Bwana, wafahamu. Ambapo, nina hakika ya kwamba kuna wengine wasiofahamu. Lakini, Baba, jalia wao—wao wajue kusudi lake. Na jalia wafahamu, Baba, ya kwamba—ya kwamba ni neema Yako kwao ya kwamba mambo haya yanafunuliwa. Nami nataka kukushukuru, Bwana, kwa bayana ya kujua mambo haya ambayo Wewe umetufunulia.

<sup>365</sup> Nami namwombea kila mmoja aliye hapa, kila mmoja ambaye amehudhuria mikutano hii. Kama kuna wengine ambao hawaamini, jalia, Bwana, wapate kuwa waamini.

<sup>366</sup> Ninawaombea wote watakaosikia Jumbe hizi kwenye kanda. Na kama ukiangukia, ambapo utaangukia, hapana shaka, katika nyumba na kwenye makazi ya wengi wasioamini ambao wataupinga; lakini, Baba, ninamwombea kila mmoja, ya kwamba kabla wao hawajasema neno lo lote la kukufuru, ya kwamba kwanza waketi chini na kuyachunguza Maandiko kwa yale ambayo yamesemwa tayari, halafu wakuambie Wewe ya kwamba wao kweli ni waaminifu na wanataka kujua kama jambo hili ni Kweli, ama si kweli. Nami ninawaombea, Baba.

<sup>367</sup> Na ninawaombea hawa ambao wamesimama kwenye kuta hizi, waliosimama nje, walioketi katika magari yao, kwa ajili ya watoto wadogo, na kwa wote ambao wamehudhuria. Na wote tu, Bwana, ninawaombea.

<sup>368</sup> Na ninaomba ya kwamba maombi yangu yatajibiwa, ya kwamba Wewe utawabariki. Kwanza, Bwana, mpe kila mmoja Uzima wa Milele. Ninaomba ya kwamba hapatakuwapo na hata mmoja wao atakayepotea, hata mmoja.

<sup>369</sup> Na sasa, Baba, hatujui ni wakati gani tukio hili kuu litakapotukia. Lakini tunapona ishara hizi zikitokea, na matukio ya Kimaandiko, yanaiwasha moto mioyo yetu kupita kiasi. Nami naomba, Baba Mungu, ya kwamba Wewe utatusaidia.

<sup>370</sup> Ninaomba ya kwamba utamsaidia mchungaji wetu mpendwa, Ndugu Neville. Mfanye, Bwana, kujaa neema na kujaa nguvu, na pamoja na ufahamu, apate kuchukua Chakula hiki lilichowekwa kwenye ghala na kuwalisha kondoo wa Mungu.

<sup>371</sup> Bwana, ninaomba ya kwamba utaondoa magonjwa kutoka kwetu. Jalia iwe kwamba, watu wanapokuwa wagonjwa, ya kwamba watakumbuka Damu iliyopo na itoshelezayo kwa yote ya Bwana Yesu iko madhabahuni, kufanya upatanisho. Nami tunaomba ya kwamba wao wataponywa mara moja.

<sup>372</sup> Nami ninaomba ya kwamba utawakinga na nguvu za Shetani, kuwavunja moyo, ama kujaribu kuwafanya waunde vikundi vilivyoyjitenga. Ama, ondolea mbali tu nguvu zote za adui kutoka kwao, Bwana. Tutakase kwa ajili ya Neno Lako. Tujalie, Bwana.

<sup>373</sup> Halafu, Bwana, ninaomba ya kwamba utanisaidia. Ni—ni—ninaanza kuzeeka, Bwana. Ninajua siku zangu haziwezi kuwa nyingi zaidi tena. Nami ninaomba ya kwamba utanisaidia, kunijalia niwe mkweli, Bwana, na mwaminifu na mnyofu, ili kwamba niweze kuupeleka Ujumbe huu umbali niliokusudiwa kuupeleka. Na itakapofikia wakati ambapo sina budi kulala, na nifike Mtoni, na mawimbi yaanze kuingia, Ee Mungu, naomba niweze kumkabidhi mtu mwingine Upanga huu wa kale ambaye atakuwa mwaminifu Kwa Huo, Bwana, naye ataibeba ile Kweli. Tujalie, Bwana. Na, mpaka wakati huo, nisaidie kuwa na nguvu na mwenye afya, na mwenye ujasiri.

<sup>374</sup> Lisaidie kanisa langu. Tubariki pamoja, Bwana. Sisi ni wako. Tunajisikia sasa ya kwamba Roho Wako yuko kati yetu. Tunaamini ya kwamba utajibu maombi yetu. Kwa kuwa, tunajikabidhi Kwako, pamoja na Neno Lako, kwa ajili ya utumishi kwa siku zetu zilizosalia duniani hapa, katika Jina la Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, Mwokozi wetu mpendwa, kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

Na- . . . (Mungu awabariki!) . . . Nampenda,  
(kwa moyo wangu wote),  
Kwani alinipenda kwanza.

Mungu akubariki, Ndugu Neville.

<sup>375</sup> [Kusanyiko linaendelea kuimba *Nampenda*. Ndugu Orman Neville anawaruhusu watu watoke kwa maombi—Mh.]

#### MUHURI WA SABA UNAENDELEA

<sup>376</sup> [Sasa hivi umemaliza kusikiliza Muhuri wa Saba asilia kama ulivyohubiriwa wote Jumapili jioni, tarehe 24 Machi, 1963 kwenye Maskani ya Branham huko Jeffersonville Indiana. Ndugu Branham hakutaka urekodishaji huu asilia utolewe. Kesho yake, Jumatatu, tarehe 25 Machi, 1963, Ndugu Branham alienda kwenye chumba cha moteli cha Ndugu Fred Sothmann

na Ndugu James Maguire ambao wakati huo walikuwa ndio waliosimamia kutengenezwa kwa kanda. Ndugu Branham akawaambia ndugu hawa, “Sitaki ujumbe huu ukasambazwe jinsi ulivyo.” Baada ya kuisikiliza kanda hiyo yeye mwenyewe, aliwaagiza hao ndugu waisimamishe kwenye mahali fulani, na mahali hapo (mwanzoni mwa aya namba 261) akarekodi sehemu mpya yenye urefu wa karibu dakika ishirini (aya 377-415). Sehemu hii mpya basi ilitumiwa badala ya jinsi ilivyoishia awali (aya 261-373). Urekodishaji huu ulikuwa ndio toleo la pekee lililosambazwa la “Muhuri Wa Saba” mpaka 1966. Baada ya Ndugu Branham kuaga dunia, halmashauri ya Shirika la Kiinjilisti la William Branham kwa kauli moja walikubaliana kuitoa ile kanda iliyorekodiwa awali huko Maskanini. Tangu wakati huo, matoleo yote mawili yamekuwako. Sasa tumeweka ujumbe huu wa ziada wa Ndugu Branham kwenye kanda moja, pamoja na “Muhuri Wa Saba” asilia. Sauti ifuatayo utakayoishia itakuwa ni ya Ndugu Branham kwenye chumba cha moteli Jumatatu, tarehe 25 Machi, 1963—Mh.]

377 Litakuwa ni jambo zuri kwamba yeye hajui kitu juu ya jambo hilo. Kwa sababu, kama angejua, basi yeye angeliiga Hilo. Hizo ndizo hila zake katika kufanya mambo.

378 Kwa hiyo, basi, Mungu ameufanya Huo ujifichike sana kwa ulimwengu mzima, hata kwa Mbingu, hivi kwamba hakuna njia ya kuuelewa Huo, ni jinsi tu Mungu atakavyo funua, Mwenyewe.

379 Sasa nawatakeni mwangalie, usiku wa leo, ya kwamba katika ule Muhuri wa Sita, kulikuwa na kusudi lenye sababu tatu la Muhuri wa Sita. Kulikuwako na kusudi lenye sababu tatu la wale wapanda farasi.

380 Kumekuwako na kusudi lenye sababu tatu katika mambo haya yote. Hilo linaturudisha kwenye tatu. Na Saba, tena, unaona, Mihuri Saba, Vitasa Saba, na kadhalika. Sasa, katika tatu na saba, ni nambari ya Mungu katika hesabu Zake za kulifunua Neno Lake.

381 Sasa unaona, kama vile katika wale—wale—wale wapanda farasi, sasa, kulikuwako na farasi watatu waliotoka. Mmoja wao alikuwa ni farasi mweupe, mmoja alikuwa ni mwekundu, mmoja alikuwa ni mweusi. Na halafu, katika yule farasi wa nne, mbona, wote walichanganywa pamoja. Unaona, kusudi lenye sababu tatu.

382 Sasa, Mungu alifanya jambo lile lile. Mungu alifanya jambo lile lile wakati alipomtuma simba Wake, ambaye alikuwa ni Neno Lake, kumkabili mpinga-Kristo.

383 Ndipo tunaona ya kwamba Yeye alimtuma ndama katika wakati wa ile—ile dhiki, yule mnyama wa dhabihu. Na katika kipindi hiki cha ile dhiki, hivyo ndivyo tu wale watu wangeweza

kufanya, ilikuwa tu ni kufanya kazi, kufanya kazi ngumu sana, na kujitolea wenyewe kama dhabihu.

<sup>384</sup> Halafu tunaona, katika wakati uliofuata, ambao ulikuwa ni wakati wa wale watengenezaji, Mungu alituma hekima ya mwanadamu, kichwa kama cha mwanadamu juu ya Mwenye Uhai, ambayo ilikuwa nguvu iliyoandamana na wale watengenezaji.

<sup>385</sup> Sasa je! umewahi kuona? Kila . . . Si ajabu ya kwamba watu wa siku hizi wangali wanaishi katika ulevi wa siku hizo, kama ilivyokuwa tangu wakati wa wale watengenezaji, kwa sababu wao wanaona mambo katika ninii—mtazamo wa kidini. Wanaona mambo kwa njia ambayo seminari imeyafundisha. Hiyo ilikuwa ni njia ya Mungu wakati mmoja, lakini hayo tumeshayapita.

<sup>386</sup> Sasa tumeingia katika wakati wa tai, ule ufunuo kufunuliwa, jambo lote zima. Sasa linganisha jambo hili na Ufunuo mlango wa 10, kifungu cha 1 hadi cha 7. Nasi tutaona hapa katika Ufunuo huu, Ufunuo hapa, 10:1 hadi cha 7, ya kwamba, “Katika siku za sauti ya Ujumbe wa malaika wa saba, huo ulikuwa umalize siri zote za Mungu.”

<sup>387</sup> Sasa tunaona, pia, katika jambo hili, ya kwamba Muhuri wa Sita, ambao sasa umefunguliwa, ulikuwa na kusudi lenye sababu tatu tatu. Sasa, haya hapa makusudi hayo.

<sup>388</sup> Jambo la kwanza, lilikuwa, ya kwamba wale wanawali waliolala ilibidi wapitie kwenye kile kipindi cha ile Dhiki kwa ajili ya kutakaswa. Ilibidi asafishwe dhambi zake za kutokuamini na kuukataa Ujumbe. Jambo hili, alifanyiwa kwake katika wakati wa ile Dhiki. Tunaona wanaishia hapa katika Ufunuo 7, kati ya sura ya 6 na ya 7 hapa, kwamba yeye alikuwa amesafishwa, na alikuwa amepewa nguo zake ndefu. Sasa, yeye si Bibi-arusi. Lakini ni kanisa, watu wasafi ambao—ambao—ambao hawakupata nafasi, labda, kuupokea Ujumbe, ama katika njia fulani kwamba wao walipofushwa na manabii hawa wa uongo. Nao—nao hawakupata nafasi, na hata hivyo wao ni waaminifu kweli moyoni. Na Mungu anajua moyo wao. Nao ndio hawa hapa wanasafishwa, katika wakati huu.

<sup>389</sup> Unauna, wakati mwingine wa kusafishwa, huo ni wa Israeli, wakati atakapokusanyika. Hilo ndilo la pili. Mungu anawasafisha Israeli katika wakati wa ile Dhiki. Kutoka katika mamilioni watakaokusanyika kule, kutakuwako na mia na arobaini na nne elfu waliochaguliwa, nao watatakaswa, pia. Mungu anawatakaswa Israeli.

<sup>390</sup> Angalia, kuna dunia nzima itakayotakaswa. Kutakuwako na vitu ambapo mwezi, nyota, na maumbile yote, vitatakaswa. Mnaona ni kitu gani? Dunia inajifanya upya, ikitakaswa, ikijifanya tayari kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Utawala wa miaka Elfu unakuja. Na, unaona, kila kitu kilicho

na uchafu wo wote ndani yake kitatakaswa katika wakati wa ule Muhuri wa Sita.

<sup>391</sup> Sasa, sasa, unaona? Kwenye kule kufunguliwa kwa Muhuri huu wa Saba, nao pia uko katika siri yenye kusudi mara tatu. Hii moja, nina. . . nitasema na nimesema, ya kwamba ni ile siri ya zile Ngurumo Saba. Zile Ngurumo Saba Mbinguni zitaifunua siri hii. Itakuwa hasa hasa ni katika wakati ule wa Kuja kwa Kristo, kwa maana Kristo alisema hakuna mtu aliyejua wakati atakaporudi.

<sup>392</sup> Uiona, wakati Wayahudi walipomwuliza jambo hilo? Unajua. . . Wakati tulipolinganisha Maandiko hapa na Mathayo 24, na Mihuri sita, Muhuri wa Saba uliachwa. Kwa sababu, unaona, Kristo alisema, “Mungu pekee Yake ndiye aliyejua; wala hata Malaika.” Si ajabu, hata haukuwa umeandikwa. Unaona, walinyamaza; hakuna kitu kilichotukia wakati huo. Malaika hawaujui Hilo. Hakuna mtu anayejua wakati atakapokuja.

<sup>393</sup> Lakini kutakuwa na—kutakuwa na Sa—Sauti Saba, za Ngurumo hizi, ambazo zitafunua ule ufunuo mkuu wakati huo. Kwa hiyo, ninaamini, kwetu sisi ambao. . . Kama hatujui, na kama sisi. . . Hautajulikana mpaka wakati huo. Lakini utafunuliwa katika siku hiyo, katika saa ile ambayo unapaswa kufunuliwa. Kwa hiyo, jambo kwetu sisi litupasalo kufanya ni kuwa na unyenyekevu mbele za Mungu, na kumtumikia, na kufanya yote tunayojua jinsi ya kufanya, na kuishi maisha mazuri, maisha ya Kikristo. Hapa, sasa, tunaona ya kwamba Muhuri wa Sita umefunguliwa kwetu; tunaona. Nasi tunajua ya kwamba huu Muhuri wa Saba hauwezi kuvunjwa kwa watu wote mpaka ile saa itakapofika.

<sup>394</sup> Sasa, kulikuwako na sababu iliyomfanya Mungu kuacha hizi Sauti Saba zingurume. Kwa sababu, hauna budi kuja, unaona. Kwa sababu ninii. . . Tunaona ya kwamba Kristo, yule Mwana-Kondoo, alikitwaa kile—kile Kitabu katika mkono Wake, Naye akaufungua Muhuri ule wa Saba. Lakini, unaona, ni siri iliyofichwa. Hakuna anayejua Hiyoy. Lakini, Hiyoy—Hiyoy, pamoja na yale aliyosema. “Hakuna mtu angejua Kuja Kwake.” Watu pia hawangejua habari za hii siri ya Ngurumo Saba. Kwa hiyo, unaona, hayo yameunganika pamoja.

<sup>395</sup> Kwa kiasi hicho, tuna ufahamu Wake, leo, kwa sababu sehemu iliyosalia yote imefunguliwa; lakini hii haijafunuliwa. Lakini nilipokuwa nimeketi kwenye chumba changu, nami nikasikia hizi. . . ama, si kusikia, hasa, lakini nikauona ukijifunua kufikia hadi kwenye hizi Ngurumo Saba. Sasa, huo ndio umbali tunaoweza kwenda, papo hapo.

<sup>396</sup> Na sasa natumaini ya kwamba kila mmoja wenu na kila mtu atamtumikia Mungu na kutenda yale yaliyo sawa. Na kumpenda Yeye, maishani mwako mwote, na kumtumikia. Na Mungu atashughulikia mengine.

<sup>397</sup> Sasa, tunaninii, katika kumalizia hapa sasa, kwa neema ya Mungu, tuna utimilifu wa siri zote za ile Mihuri Sita ambayo ilikuwa imetiwa muhuri, nasi tunafahamu na tunajua hapa ya kwamba Muhuri wa Saba shautafahamika kwa watu wote.

<sup>398</sup> Sasa, Kuja Kwake, kwenye ile saa ya Kuja Kwake, wakati yale maangamizi ya dunia, mnajua. Yeye alisema pale, “Dalili ya kuja kwa mwisho wa ulimwengu itakuwa ni nini?” Katika Mathayo 24, pale ambapo wao walimwuliza Yeye swali hilo. Yeye aliliandea jambo hilo. Yeye alisema habari za Israeli kukusanyika kama taifa, katika aya ya 31, ya Mathayo 24:31. Lakini baadaye Yeye akaanza kutoa mifano, unaona. Halafu unaona ile... “Jifunzeni mfano wa mtini. Mkiuona ukichipua matai majani yake, mbona, mnajua msimu wa kupukutika majani umekaribia. Ndipo basi mtakapoona jambo hili likitukia, basi mjue wakati umekaribia.” Unaona, Israeli inakusanyika katika nchi yake yenyewe. Lakini, unaona, Yeye aliacha ufunuo wa huu Muhuri wa Saba.

<sup>399</sup> Na hapa, wakati ule Muhuri wa Saba, wakati Yeye alipoufunua, Yeye aliacha tena, unaona. Kwa hiyo tunaona ya kwamba ni siri kabisa, kwa hiyo ile saa haijatimia bado kwa ile siri kujulikana. Kwa hiyo, tumekwenda umbali huu, na yaliyosalia yatajulikana moja kwa moja wakati ambapo Yesu atatokea duniani tena, kwa ajili ya Bibi-arusi Wake, ama cho chote kitakachotukia wakati huo. Sasa, mpaka wakati huo, hebu sote na tuombe tu, tuishi maisha mazuri, manyofu, ya Kikristo, tukikutazamia Kuja Kwake.

<sup>400</sup> Na sasa kama ikitokea kwamba kanda hii itaangukia kwenye mkono wa watu fulani mahali fulani, usijaribu kufanya namna fulani ya itikadi kutoka kwake. Jambo pekee unalopaswa kufanya, endelea tu kumtumikia Mungu. Kwa sababu, siri hii kuu mno ni kuu sana hata Mungu asingemwacha Yohana kuiandika. Ilinguruma, lakini Yeye... akijua jambo hilo, akituahidi ya kwamba ungefunguliwa. Lakini, mpaka wakati huu, haujafunguliwa.

<sup>401</sup> Na sasa tuna shukrani kwa Mungu kwa ajili ya yale Yeye aliyotuonyesha. Nimekuwa nikiketi chumbani mle kwa siku nane. Na ule Ujumbe ambao ndiyo tu nimalize kuwaelezea, wengi wenu hapa mtafahamu. Nami niliahidi ya kwamba kulikuwako na jambo fulani lililokuwa likiendelea, la kiroho, wakati wote, ambalo nilikuwa na hakika mlikuwa mnalikosa. Nalo ndilo hili hapa; ni kuthibitishwa kikamilifu kwa hii tafsiri ya Maandiko kwamba imetumwa na Mungu.

<sup>402</sup> Kwa sababu, hata kabla hatujaliingilia jambo hilo, nami niliondoka kwenda magharibi, Bwana alinionyesha ono siku moja, kama saa nne, asubuhi moja. Nami nikaja na kulielezea hapa, ya kwamba nilikuwa nimeliona; sikujuu ilikuwa ni nini. Ilikuwa ni kundi la Malaika saba. Tutakumbuka jambo hilo.

Mtalipata kwenye kanda, inayoitwa, *Ni Saa Ngapi, Bwana?* Vema, sasa, hao ndio mnaowaona hasa kabisa sasa hivi. Wale Malaika saba . . . Nilikuwa kule magharibi.

<sup>403</sup> Mnakumbuka, wale wajumbe wadogo sana; walienda mashariki. Wale wajumbe wa pili, wale hua, ndege wakubwa kidogo, walienda mashariki. Na kisha nikaangalia . . . Walikuwako pamoja nami, wakati wote. Hiyo ulikuwa ni ni ule Mvuto wa Kwanza na wa Pili.

<sup>404</sup> Sasa, wa Tatu ulikuja kutoka magharibi, wakienda mbele kwa mwendo wa kasi sana, Nao wakanitwaa juu. Hiyo ilikuwa ni kurudi mashariki, pamoja na siri ya hii Mihuri Saba. Kama tu vile ilivyosema katika—katika ndoto ya Junior Jackson, ambayo Bwana alinijalia kumfasiiria pale, “Kule ndani ya hiyo piramidi, kulikuwako na Jiwe jeupe ambalo halikuwa limeandikwa.” Hiyo ndiyo sababu ilinibidi kwenda magharibi, kuungana na Ujumbe wa Malaika hawa, kurudi hapa na kuufunulia kanisa. Kumbukeni, nilisema, “Mambo mengine yanayotukia yatakuwa ni hapa kanisani.” Hiyo ni sawasawa kabisa.

<sup>405</sup> Jambo ligine, ninataka muone yale yaliyotukia. Na Kama mnasikiliza kanda, ya *Ni Saa Ngapi, Bwana?*, utaona ya kwamba Malaika mmoja alikuwa wa kipekee sana kwangu. Hao wengine walionekana kama wa kawaida. Lakini Malaika huyu alikuwa Malaika wa kipekee. Alikuwa mkono wangu wa kushoto, katika kundi lile lililo katika mfano wa piramidi.

<sup>406</sup> Na, kumbukeni, ilikuwa ni humo ndani ya lile piramidi, ambapo ule Mwamba mweupe wa siri haukuwa umeandikwa. Nao hao Malaika wakanichukua kuniingiza kwenye hiyo piramidi wao Wenyewe, ikiwa zile siri za Mungu zinajulikana na Wao peke yao. Na, sasa, Hao walikuwa ndio Wajumbe wale waliokuja kuifasiri ile piramidi, ama huo Ujumbe wa zile siri za hii Mihuri Saba ambayo inakaa ndani ya lile Piramidi.

<sup>407</sup> Sasa, yule Malaika, aliyekuwa kushoto kwangu, angekuwa hasa ndiye wa mwisho, ama Malaika wa saba, kama tungewahesabu kutoka kushoto kwenda kulia. Kwa sababu, Yeye alikuwa kushoto kwangu; mimi nikimwangalia, kuelekea machweo ya jua, Yeye akija kuelekea maawio ya jua, angekuwa upande wa kushoto. Kwa hiyo, huo ungekuwa ndio Ujumbe wa malaika wa mwisho, wa kipekee sana mno. Kumbukeni jinsi nilivyosema alielekeza ninii Yake, aligeuza kichwa chake kuelekea nyuma; na mbawa zake kubwa, zilizochongoka; na jinsi alivyoruka akanijia moja kwa moja. Sasa, huyo ndiye huu Muhuri wa Saba. Lingali ni jambo la ajabu sana. Nasi tuna- . . . Hatujui Huo ni nini, bado, kwa sababu hauruhusiwi kuvunjwa.

<sup>408</sup> Lakini sasa, kila mmoja wenu mkutanoni ameona jambo hilo, umekuwa ni mkutano wa namna gani! Kila mtu alionekana kana kwamba yuko chonjo. Na kila mtu akisimama karibu na hapa, saa saba, saa nane alasiri, akingojea milango ifunguliwe,

na kuja huku mbele. Wakisimama kando ya kuta; viungo vya mwili vinauma, na kila kitu.

<sup>409</sup> Ni kitu gani? Ilikuwa ni Roho Mtakatifu akiwatuma hawa Wajumbe, nao wamekuwa wakitufunulia Hilo. Na basi angalia jinsi ambavyo limekubaliana na Neno, kabisa.

<sup>410</sup> Na halafu kuwaacha ninyi nyote mjue ya kwamba hii ni Kweli, Yeye alilitabiria kama—kama miezi miwili sasa, ama zaidi, kabla halijatendeka kamwe. Kwamba, nilipoenda magharibi, bila kulijua Hilo; nikarudi hapa na fasiri yake kama vile Yeye alivyoitoa. Sasa kumbukeni, katika ono, Yeye hakuniambia kamwe jambo hata moja katika ono wakati aliponitwaa juu. Niliogopa, niliogopa nitakufa, kuuawa katika mlipuko. Unaona, Wao hawangeweza kufanya jambo hilo.

<sup>411</sup> Fasiri yake ilikuja wakati tu nilipoihitaji, hiyo ilikuwa mle chumbani, nami niliitoa kama tu Yeye alivyoniipa.

<sup>412</sup> Sasa, mnaona, marafiki, maono hayashindwi. Hayo daima ni makamilifu. Hayo ni ya kweli tu kabisa.

<sup>413</sup> Sasa, lile ono, pamoja na Neno, pamoja na historia, pamoja na nyakati za kanisa, na kila kitu, vimeungana pamoja. Kwa hiyo, ningeweza kweli kusema, ya kwamba, ni juavyo mimi kabisa kabisa, na kulingana na Neno la Mungu, na lile ono, na ule ufunuo, na fasiri hii ni BWANA ASEMA HIVI.

<sup>414</sup> Sasa, Bwana na awabariki ninyi nyote, kila mmoja, sana sana, tunaposimama sasa na kuimba wimbo huu mzuri wa zamani wa kanisa. Mungu awabariki, kila mmoja. Amina.

<sup>415</sup> [Ndugu Branham anaongeza mistari hii minne inayofuata, iliyotolewa kutoka kwenye aya ya 374 ya Ujumbe wake wa jana jioni, tarehe 24, Marchi, 1963.—Mh.]

Na- . . (Mungu awabariki!) . . . nampenda,  
(kwa moyo wangu wote),  
Kwani alinipenda kwanza.

Mungu akubariki, Ndugu Neville.





*UFUNUO WA MIHURI SABA*  
(The Revelation Of The Seven Seals)

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kutoka tarehe 17 Machi mpaka tarehe 24 Machi, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, na Muhuri wa Saba ukaendelea tarehe 25 Machi katika Hoteli ya Sherwood. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamilifu zaidi, kitabu hiki kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

Haki zote zimewekwa. Kitabu hiki hakiwezi kuuzwa, kuchapishwa tena, ama kufasiriwa katika lugha zingine, ama kutumiwa kwa kuchangisha fedha bila barua ya kuruhusia ya William Branham Evangelistic Association. Kilichapishwa tena katika mwaka wa 2006.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)